Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 173 | JUMADUTHTHANI1434AH | APRILI 2013 | SHAHADAT 1392 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika Mwenyezi Mungu anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa adili; bila shaka mauidha anayowatoleeni Mwenyezi Mungu ni mazuri sana; Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye, Aonaye.' (4:59)

'Uongozi ni dhamana'

Asisitiza Kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani

Na Mwandishi wetu

Hadhrat Khalifatul Masih (a.t.b.a) alianza hotuba ya Ijumaa kwa kusoma aya ifuatayo:

'Hakika Mwenyezi Mungu anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa adili; bila shaka mauidha anayowatoleeni Mwenyezi Mungu ni mazuri sana; Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye, Aonaye.' (4:59)

Kama ambavyo Jumuiya nyingi zinafahamu, huu ni mwaka wa uchaguzi katika Jumuiya yote. Chaguzi za maAmeer, masadr na viongozi wengine hufanyika kila baada ya miaka mitatu. Katika baadhi ya sehemu chaguzi hizi zimeshaanza tayari. Majlis e Intikhab ipo katika Jumuia kubwa kubwa ambayo huwateua viongozi. Wakati ni muhimu kufanya uchaguzi kwa ajili ya kuendesha shughuli za Jumuiya kwa mfumo unaoeleweka, ni muhimu zaidi pia kumchagua mtu anayefaa kuitendea haki ofisi aliyopewa. Kwa hakika hili ni muhimu sana kiasi hiki kwamba Qur'an Tukufu inauelekeza uzingativu wetu kwenye jambo hili hili, inapoelezea ni aina gani ya watu wanatakiwa kuchaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali. Vile vile inazungumza na viongozi hao walioshika nyadhifa mbalimbali kwamba kuwa na wadhifa tu hakutoshi, haki za ofisi husika zinahitaji kutekelezwa na inapokuwa hazitekelezwi mtu hupata ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.ba, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Duniani

Wajibu wa kwanza uliotajwa katika aya hiyo hapo juu ni kwamba kuwa na wadhifa ni dhamana; kwa hiyo wachagueni wale ambao ni bora zaidi kwa muono wenu. Tafakarini kama wanastahili na wanao uwezo wa kushikilia wadhifa husika au la. Kadiri wadhifa unapokuwa mkubwa ambao kwa ajili yake mmekusanyika ili kutoa maoni yenu kwa Khalifa wa zama, ndivyo mnavyohitajika kufikiri kwa makini zaidi na kufanya maombi.

Kura hazipaswi kupigwa kwa msingi ya undugu, urafiki au ukabila na mtu. Mwenyezi Mungu sio tu atawataka kujibu viongozi, bali, waliopiga kura pia , watatakiwa kujibu kwamba kwa nini hawakupiga kura zao vizuri. Aya hii inaelekeza kwamba ikiwa mtu hana taarifa za kutosha juu ya wale wanaotakiwa kupigiwa kura, basi na aombe kwa Mwenyezi Mungu kwamba amfanye aelekee kumpigia kura yule ambae mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu ndiye anayefaa zaidi. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Asikiae, Aonae na anazo habari hata juu ya yale yaliyomo nyoyoni, kwa hiyo hakuna awezayo kumdanganya. Mwenyezi Mungu husaidia pale ambapo kundi la waaminio watapiga kura zao baada ya kufanya maombi kwa moyo huu ili kuwachagua viongozi mbalimbali.

Ni desturi ya Jumuiya yetu kwamba kabla ya shughuli

Endelea uk. 3

Islam Ahmadiyya yazidi kung'aa Uhispania

Msikiti mwingine wafunguliwa Valencia

Na Jamil Mwanga na Abdulrahman Ame, Dar es Salaam

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alitoa hotuba ya Ijumaa tarehe 29 Machi, 2013 katika msikiti mpya wa Baitur-Rahman uliojengwa mjini Valencia, Uhispania. Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisoma aya zifuatazo:

'Na (kumbukeni) Ibrahimu alipoiinua misingi ya Nyumba, na Ismaili pia, (wakaomba):

Endelea uk. 2



Masjid Baitur Rahman Valencia, Uhispania

Mungu Ibariki Kenya, Ibariki Afrika Mashariki na Afrika yote

Na Pazi Mazongera
Dar es Salaam

Nchi ya Kenya imeandika historia mpya katika siasa za nchi hiyo yenye uchumi mkubwa katika Afrika ya Mashariki. Mnamo tarehe 9 Aprili 2013 ilimpata Rais wake mpya, si mwingine ni Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyata. Tuna kila sababu ya kuwapongeza wananchi wa Kenya, kumpongeza Rais mpya na Makamu wake Mheshimiwa William Rutto. Kubwa zaidi tunawapongeza wakenya kwa kujenga heshima ya nchi hiyo, Afrika ya Mashariki na Afrika yote kwa kufanya uchaguzi wa amani na kuendeleza amani hiyo hata pale matokeo yalipopingwa Mahakamani, wana Kenya walikuwa watulivu kusubiri matokeo ya Mahakama kwani ndiyo njia ambayo watu wa Kenya walikubali ndiyo itumike. Katika hili tunawapongeza sana kwani kulinda amani ni jambo



Uhuru Muigai Kenyata Rais wa Kenya

la thamani kuliko kupata Rais ambaye walimpenda wakati kuna vita na mauaji.

Tumepata faraja pia kupata habari kuwa mpinzani wake mkuu Mheshimiwa Raila Odinga ambaye hakuwepo nchi Kenya wakati wa sherehe za kuapishwa

Endelea uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SOMA

Neno la kwanza liliteremshwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni neno 'Soma'. Hapana shaka neno hilo limebeba ujumbe mzito. Ilikadiriwa ya kuwa maendeleo na mafanikio ya binadamu yatajengwa kwenye jiwe hili la pembeni ambalo kwa bahati mbaya kwa hivi sasa linakataliwa na Waashi.

Utamu wa kusoma ili kuyafahamu mazingira yako zaidi ili uweze kuyatawala, utamu huo kwetu imegeuka shubiri. Kwa ujumla wa maneno hatusomi.

Utafiti unafanywa na matokeo ya utafiti yanaweza kuwekwa mezani kwa kiongozi na hayasomi matokeo yake tunarudia jambo lile na aghalabu tunaunda tume kuchunguza jambo ambalo liko bayana mezani kwetu. Hata hotuba inapotolewa dalili zote za kuonesha haikuwepo jitihada ya kusoma inakuwa bayana.

Lakini utamaduni wa kutopenda kusoma unaanzia shuleni. Je Waalimu wetu wanao utamaduni wa kumuona ameshika kitabu anasoma, watoto wataiga mfano kutoka wapi? Wazazi nyumbani wanayo maktaba angalau ndogo? Je wazazi wanapanga siku moja ya kuwapeleka watoto wakaazime vitabu maktaba? Ni watanzania wangapi ambao utawaona wanasoma kitabu. Katika hali ya namna hiyo mtoto anakuwa akitambua kuwa kusoma ni kwa ajili ya mitihani tu na mambo yanakuwa mabaya zaidi uchochoro ukipatikana wa kununua mitihani na kupatikana kwa nafasi za mitihani inayoitwa feki.

Mwenyezi Mungu Anasema tembeeni katika ardhi. Na maana ya kutembea ni kujifunza. Nchini Marekani bibi kizee mwenye umri wa miaka themanini anaingia maktaba anaazima vitabu na anavisukuma kwenye kigari hadi nyumbani kwake. Tembea sehemu yoyote ya Japan, kwenye treni, kwenye ndege, kwenye basi kila mtu utamuona kainama katika kitabu chake. Mapenzi ya kusoma ndiyo yanayotakiwa.

Kutokana na hali halisi ya nchi yetu, hatukushangaa hata kidogo tulipopata taarifa za matokeo ya kutisha ya kidato cha IV. Daima binadamu huvuna alichopanda.

Unatarajia nini katika shule ambazo hazina Maktaba? Lipi la ajabu katika shule zisizo na Maabara? Watapitaje katika mtihani mahali ambapo Mwalimu ana mlima wa madaftari ya kusahihisha? Na nyumbani hakuna umeme na ni mwezi wa tatu sasa hajapata mshahara? Unategemea nini katika mfumo ambao wanafunzi wana uhakika wa kupata karatasi za mitihani kabla ya mitihani? Lipi la ajabu wakati bajeti ya elimu ni finyu? Muujiza gani utatokea katika shule zisizo na wakaguzi? Hayo yote ukiyachanganya na 'uhasama' wa kutopenda kusoma inakuwa kama mtu aliyeruka kutoka kwenye moto na kutumbukia kwenye kikaango.

Hatujachelewa sana. Tuanze kujenga mapenzi ya kupenda kusoma. Tukifaulu kupata hilo tunaweza kusema bila wasiwasi, tafuta ufalme wa mapenzi ya kupenda kusoma na kila kitu kitaongezwa kwako.

Waandishi wetu nao wachonge kalamu zao ili watuletee yale yanayoelimisha na kuburudisha. Jamii nayo isibaki nyuma iwape taadhima na iheshimu kazi zao. Kuwasifu waandishi wakisha kufa haitasaidia sana. Wakati umefika wa kuwaheshimu waandishi wetu, kuwaenzi na kuwashukuru kwa mchango wao. Si jambo baya kama siku moja maalumu inatengwa ya kuwakumbuka waandishi wetu. Na wala hatutakuwa tumefanya kioja. Nchini nyingi duniani zinao utamaduni wa kuwaenzi waandishi wao. Jambo lolote lililo zuri si vibaya kuliiga.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jumuiya, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jumuiya Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Msikiti mwingine wafunguliwa Valencia

Kutoka uk. 1

Ee Mola wetu, Utupokelee, hakika Wewe ndiwe Mwenye kusikia, Mwenye kujua.
Ee Mola wetu, Utufanye tuwe wajitupao Kwako, na miongoni mwa wazao wetu pia Uwafanye watu wajitupao Kwako. Na Utuonyeshe njia za ibada yetu na Utuelekee; bila shaka Wewe ndiwe Mwelekevu, Mrehemevu. ' (2:128 – 129)

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a alisema sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kujenga msikiti mwingine nchini Uhispania. Aliongeza kwamba takriban miaka 7 iliyopita alisisitiza kuhusu umuhimu wa kuwa na msikiti mwingine nchini Uhispania baada ya ule wa Basharat, Pedroadbad. Iliamualiwa wakati huo kwamba msikiti mwingine ujengwe Valencia. Ingawaje idadi ya wanajumuiya katika eneo hili ni 130 tu lakini umuhimu wa kujenga msikiti mwingine hapa unatokana na ukweli wa historia ya eneo hili. Ahmadiyya Jama'at imewezeshwa kujenga msikiti mwingine baada ya kipindi cha miaka 30 tangu ulipojengwa msikiti wa mwanzo. Katika kipindi hiki Waislamu wengi wamehamia Uhispania na wamejenga misikiti. Milango hii imefunguliwa kwao baada ya ujenzi wa msikiti wetu wa Basharat. Kwa Hakika Jumuiya Ahmadiyya iliwezeshwa kujenga msikiti baada ya miaka 700 tangu maanguko ya waislamu kwenye nchi hii. Kwa sasa idadi ya Waislamu nchini Uhispania inafikia milioni moja na inakadiriwa kwamba ifikapo mwaka 2030 idadi hii itakuwa imeongezeka kwa 80% na itafikia milioni mbili. Miaka 30 iliyopita Uhispania ilikuwa na Waislamu wachache sana. Idadi kubwa ya Waislamu wa Uhispania ni wa asili ya Afrika Kaskazini na pia inaweza kusemwa zile familia za Kiislamu za karne nyingi ambazo zililazimishwa kuingia kwenye Ukristo lakini waliacha imani zao na kurudi katika uislamu. Kwa fadhili za Allah leo kuna waislamu wengi Uhispania na ongezeko hili limetokana na kuwepo kwa Jumuiya Ahmadiyya nchini Uhispania. Hata hivyo, uislamu wa kweli utaonekana nchini Uhispania pale ambapo watumishi wa Masihi wa Muhammad wataelewa dhima yao na wataelekaza nguvu zao katika kufikisha ujumbe wa Ahmadiyya kwa kila mtu wa nchi hii. Baadhi wanaweza kuhoji kwamba kuna Waahmadiyya wachache hapa, wanawezaje kuufikisha ujumbe kwa kila mtu? Hata hivyo, kama mtu akikusudia na akafanya juhudi, hilo linawezekana. Mipango imekuwa ikifanywa mara kadhaa juu ya hili lakini utekelezaji haukufanyika. Mipango iliyotolewa na Markaz na Khalifa Mtukufu na kwa hakika tangu Khalifa Mtukufu wanne r.a. haikuwa ikitekelezwa.

Msikiti wa Basharat upo karibu na njia inayoelekea Cordoba. Kama mkakati ungefanywa, Jamaat yetu ingaliweza kuenezwa kutoka eneo hilo. Jamaat zingine ingawa ni wachache, wamefikisha ujumbe wetu kwa watu wengi kwa njia ya vipeperushi. Watu wengi kutoka maeneo mengine wamefika kuuona msikiti wa Basharat. Endapo kazi ingefanyika kwa jazba na shauku, Jamaat ingaliweza kufahamika. Kama waislamu wengine wameweza kuwarejesha katika Islam 'waislamu wa mwanzo wa Uhispania' wapatao 20,000, kwa nini hilo lishindikane kwa tabligh yetu ambayo imesheheni ujumbe wa kweli wa Islam. Kwa hakika, tumefungua milango hii lakini hatukutumia njia hizi kwa jazba na shauku huku wengune wakizitumia vyema fursa hizi. Viongozi wa Jamaat katika kila ngazi nchini Uhispania watambue majukumu yao, waweke malengo na kujitahidi kuyafikia.

Picha ya kweli ya Islam tunayoitangaza inatakiwa ienezwe kote duniani. Kizazi kinachotokana na familia za mwanzo za Kiislamu hapa Uhispaniawanatakiwa wafahamishwe kwamba huu ni wakati wa kurejesha malipo ya ukatili uliofanywa dhidi ya mababu zao (yaani kuirejesha Uhispaniana watu wake kwenye Islam). Hata hivyo, malipo hayo hayatakiwi yafanywe kwa kutumia nguvu kwani Islam inafundisha kwamba **'Hakuna karaha katika dini;'** (2:257). Aidha, Mwenyezi Mungu anafundisha kwamba uadui wa watu usiwafanye mkaacha uadilifu, **'Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa, na Mcheni Mwenyezi Mungu.…'**(5:9). Ni uchamungu tu ndio umfikishao mtu karibu na Mwenyezi Mungu. Aidha, hakuna suala la uadui hapa; kwani hawa ni raia wenzao na inabidi wafikishiwe ujumbe wa Islam wa mapenzi na amani. Inabidi kwanza tuwaeleze uzuri wa mafundisho ya Islam na kisha tulipe kwa kujaribu kuziteka nyoyo kupitia mafundisho haya mazuri ya Islam. Nyoyo zilizolazimishwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu zipandikizwe Mapenzi ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na mapenzi Muhammad s.a.w. kuwa Mtume wake. Mapenzi ya Mwenyezi Mungu ambaye sifa yake ya huruma inazifunika sifa zake zote nyingine na mapenzi ya Mtume wake ambaye ni Rahmatullil A'lameen (Rehema kwa walimwengu). Familia hizi kongwe za kiislamu inatakiwa zitafutwe na juhudi maalumu ya kuzijengea mapenzi ya dini zifanyike na kisha wenyewe wafanywe kuwa wahubiri wa imani.

Sababu ya Huzur a.t.b.a kuchagua eneo la Valencia kwa ajili ya kujengwa msikiti wa pili ni kutokana na historia ya Uhispania inayotupasha kwamba zama ambapo Mfalme na Malkia wakatili walipowalazimisha waislamu kwa mabavu kuingia katika Ukristo, pamoja na mateso makubwa, Valencia ndio mji ambako Kiarabu kiliendelea kuzungumzwa. Waislamu wa Valencia waliendelea kwa uwazi kumwabudu Mola wao na walidumu katika mafundisho wakati ambapo waislamu wa maeneo mengine ya Uhispania hawakuweza kudhihirisha imani yao. Pindi mfalme alipoamuru waislamu wafukuzwe na kuondokaUhispania, kwenye miaka ya 1600, waislamu wa Valencia walikuwa ndio wa kwanza kufukuzwa kwa sababu ya kuendelea kwao kutekeleza mafundisho ya imani yao. Waislamu wa Uhispania nyakati hizo hawakuwa na uwezo kifedha na walifukuzwa kwenye miji mikubwa na kusambaa kwingineko. Hatimaye, wafalme mbalimbali walitawala Uhispania. Jeshi la Italia nalo pia lilifanya ukatili mkubwa kwa Waislamu, liliwafukuza watu wazima na kuwachukua watoto wao kwa nguvu na kuwaingiza kwenye familia za Kikristo ambako walifanywa kuwa watumishi kama watumwa. Watoto hawa walikatazwa kumwabudu Mungu mmoja badala yake walilazimishwa kushika imani ya utatu. Leo ni jukumu letu kwa mara nyingine kuwafanya wawe wenye kumwabudu Mungu mmoja. Pia tunatakiwa kuufikisha ujumbe huu kwa wengine, kutokana na huruma yetu kwa wanadamu, tunatakiwa tuwapendelee kama tunavyozipenda nafsi zetu. Juhudi hii ya jambo hili ifanywe hususan katika eneo hili kwa sababu hapa Uislamu umedumu. Kwa hakika, hapa Waislamu hawakufukuzwa karne saba zilizopita bali ni karne nne zilizopita**.**

Hakuna shaka kwamba baada ya kuongoza kwa karne nyingi, maanguko ya waislamu yalisababishwa na ugomvi na fitna miongoni mwao. Wakati huo sio yule aliyeitwa Khalifa tu bali mfalme na watendaji wengine pia, wote hakuna aliyejali majukumu yake. Kila mtu alikuwa na kundi lake na matokeo yake kila kitu kikafanywa kuwa ni kwa ajili ya maslahi binafsi. Sasa hizi ni zama za Ukhalifa wa Masihi Aliyeahidiwa, na hivyo ni jukumu la wafuasi wake kuhakikisha kwamba wanairejesha heshima ya Islam iliyopotea na wanaifikisha kwa watu ile imani: 'Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume Wake na Mtumishi wake.' Mwenyezi Mungu ametuwezesha kujenga msikiti katika eneo hili na tumepata eneo mwafaka kwa ajili hii. Msikiti uko sehemu ambayo unaonekana vizuri kwenye barabara kuu. Hili ni eneo linaloheshimika na tunao

Endelea uk. 4

‘Uongozi ni dhamana’ - Khalifa Mtukufu

Kutoka uk. 1

yoyote ikiwemo ya uchaguzi maombi hufanyika kwanza. Mchakato wa uchaguzi unaofanyika kwa ukweli wa moyo kamili hubarikiwa na Mwenyezi Mungu. Kura zipigwe bila kufuata matakwa binafsi ya mtu na mahusiano. WaAhmadiyya wa muda mrefu wanafahamu jambo hili na wapya na vijana wanapaswa pia kutambua kwamba chaguzi ni mchakato wa kutoa mapendekezo; uamuzi wa mwisho hufanywa na Khalifa wa zama.

Katika hali fulani fulani pamoja na mtu kupata kura nyingi, wadhifa anapewa mwingine. Inapaswa pia kueleweka kwamba Ameer wa nchi anayo mamlaka ya kuidhinisha uteuzi wa baadhi ya viongozi na anayo pia mamlaka ya kumteua mtu ambaye hakupata kura nyingi.

Hata hivyo maAmeer wanatakiwa kwa ujumla kuheshimu uwingi wa kura. Kwa ajili ya Uingereza na nchi za Ulaya, Amerika, Canada na Astralia (maAmeer) wanaangalizwa kwamba ingawa kanuni zinamruhusu Ameer kumchagua mtu tofauti na yule aliyepata kura nyingi, katika uchaguzi wa mwaka huu endapo watahitaji kufanya mabadiliko yoyote wawasiliane kwanza na Khalifa ili kupata idhini yake.

Hata hivyo, Pakistan na India waendelee na chaguzi zao kama mwanzo sawa na kanuni.
Majlis Amila ya kila nchi inaidhinishwa na Khalifa wa zama kwa vyovyote vile.

Aya hii inasema kwamba: ‘…zirudisheni amana kwa wale wanaozistahili...’ jambo hili linawahusu viongozi vilevile. Watu wanaoteuliwa na sio kuchaguliwa, kushika nyadhifa mbalimbali kwa mfano katibu wa Rishta Nata na kazi nyingine wapangiwazo watu katika idara mbalimbali; wanapowateua watu kushika nafasi kama hizi maAmeer na masadr hawatakiwi kufuata mapenzi yao binafsi au mahusiano. Kinyume chake wanapaswa kuwapima kikamilifu wanajumuia na kumchagua mtu anayeonekana bora zaidi; vinginevyo itakuwa ni upendeleo wa ujamaa ambao Islam inaukataza. Hata hivyo, ikiwa mtu atamchagua mtu kwa msingi unaostahiki, wale waliozoea kutoa malalamiko, watatoa malalamiko ya bure. Wanatakiwa waache kufanya hivyo. Sio dhambi kuwa karibu na Ameer au kiongozi kiundugu na hili halitakiwa kuwa sababu ya kumzuia mtu kuitumikia Jumuiya. Jambo hili limefafanuliwa kwa sababu baadhi ya watu hutoa manung’uniko kama hayo.

Mwenyezi Mungu anasema katika aya hii ‘… mhukumu kwa adili...’ Ikiwa ujamaa na upendeleo utafanyika haki haitatendeka na mambo yote yatapoteza baraka. Maamuzi ya haki na ya usawa yapaswa kufanyika na viongozi kuhusiana na kila Mwanajumuia. Isiwe kwamba ikiwa mtu ni rafiki wa fulani au kutoka katika familia fulani basi anatendewa tofauti wakati maamuzi yasiyostahili yanafanywa kwa wengine. Mambo kama haya huleta mashaka katika Jumuiya. Endapo Khalifa wa zama ameagiza ripoti juu ya jambo fulani, ripoti sahihi ipelekwe kwake kwa kuwa imeagizwa ‘… mhukumu kwa adili...’, ikiwa ripoti isiyo sahihi itapelekwa kuna uwezekano kwamba kwa kutumia ripoti hiyo Khalifa wa zama atafanya uamuzi usiokuwa sahihi na kwa hivyo akashiriki katika dhambi ya wale waliopeleka ripoti potovu.

Kila kazi, kila huduma ambayo inahitajika mtu aitoe, itolewe kwa umakini na uaminifu. Kushika ofisi sio ukubwa, kwa kweli ni dhamana kubwa ambayo yapaswa kutekelezwa kwa maombi. Mwenyezi Mungu anasema kwamba Yeye ni ‘… Asikiae, Aonae...’ Husikiliza Maombi hususan maombi yale yanayofanywa kumuomba msaada katika kutimiza amri Zake. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu humchunguza yule anayepiga kura, Huwachunguza pia wale wanaoshika madaraka. Kama Viongozi hawashiki adili, Mwenyezi Mungu anasema atawauliza. Ni jambo la kuleta hofu kubwa kule mtu kupewa dhamana ya kuitumikia Jumuiya katika kazi yoyote.

Watu wanapenda cheo. Laiti wangelijua ukubwa wa jukumu hili na ambalo kushindwa kulitimiza hupelekea ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, kila mmoja angelimpita mwenzake katika kufanya istighfar usiku na mchana. Kila kiongozi apaswa kutambua kwamba baada ya kuchaguliwa na kuthibitishwa hayuko huru, kwa kweli analazimika kujitolea kwa uwezo wake wote na kushindwa kufanya hivyo kwaweza kusababisha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.

Kila kiongozi anatakiwa kutimiza haki ya kila mwanajumuia mmoja mmoja na hali kadhalika haki ya Jumuiya kwa ujumla. Kila kiongozi atafakari kwamba nafasi aliyoshikilia haiiathiri vibaya Jumuiya au kuliharibu jina la Jumuiya. Mifano ionyeshwe ya utekelezaji wa hali ya juu wa majukumu ya kidini na yale ya kidunia vilevile. Haiwezikani kusemwa kwamba jambo fulani ni la mtu binafsi yake, na halina uhusiano na Jumuiya, na kwa hiyo mtu anaweza kufanya kama atakavyo mwenyewe.

Kila kiongozi anatakiwa kutambua kwamba nafsi yake imefungamana na Jumuiya kwenye kila jambo. Msimamo huu ushikiliwe na kila kiongozi na wale wanaoshikamana na msimamo huu ndio wachaguliwe. Kwa maneno mengine, kura wapigiwe wale walio na kiwango cha juu cha Taqwa.

Ikiwa tunadai kwamba baada ya kumpokea Imam wa zama tumekuza kiwango chetu cha Taqwa na tunatimiza ahadi zetu kuliko wengine, basi majukumu tunayodaiwa na Jumuiya lazima yatekelezwe kwa umakini unaostahili.

Mwenyezi Mungu anasema katika Qur’an Tukufu: ‘Na ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao’ (23:9). Amri hii inapaswa kuzingatiwa na kila mmoja katika eneo lake. Amana hazipaswi kuheshimiwa kijuu juu tu. Bali mtu atekeleze wajibu wa kazi yake kwa kina na umakini. Wachaguliwe watu wale ambao ni wazingativu wa kazi zao na wale wanaochaguliwa nao wanatakiwa kufanya vizuri kadiri ya uwezo wao. Nikiongozi ndiye anayetakiwa kuishika ahadi ya ‘kutanguliza dini juu ya dunia’ zaidi kuliko wengine. Ni kinyume na mafundisho ya Islam kutamani uongozi, hata hivyo ikiwa mtu anataka kutoa huduma au amepewa dhamana ya utumishi, basi ikimbukwe ya kwamba hilo halitotimia mpaka mtu atimize ahadi yake kikamilifu.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaelezea suala la kutimiza ahadi:
‘Allah Mwenye Enzi amesema katika aya hii adhim: ‘Na wale ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao’... wale ambao sio tu wanayo adhama ya kuyashinda matamanio ya Nafsi Ammarah (nafsi inayochochea maovu) na kwa hiyo wameyashinda matamanio yake, bali wanajaribu kadiri inavyowezekana kuzingatia kila hali ya amana zote na ahadi zote za Mungu na viumbe wake na wanajaribu kutembea katika njia nyembamba ya Taqwa. Wanang’ang’ana katika njia hii kadiri nguvu zao zinavyowawezesha... Neno ‘Ra’oon’ (ahadi) katika aya hii... limetumika kwa msemo wa Kiarabu ukimaanisha hali ile ya mtu anapotaka kufuata njia za ukamilifu katika jambo kwa uwezo wake wote na anatamani kuitekeleza kila nukta yake na hataki kubakisha hata chembe. Kwa hiyo, aya hii inamaanisha kwamba waaminio hutembea katika njia nyembamba za Taqwa kwa kadri ya uwezo walio nao na hawatamani kubakisha chochote kuhusiana na dhamana na ahadi na wanazingatia hilo juu ya kila mtu. Hawaridhiki kwa kujiona kwa ujumla kwamba ni wakweli na waaminifu, bali wanakuwa na hofu kwamba wasije wakafanya kosa la kutotimiza ahadi. Wanaendelea kutafakari kwa kina juu ya wajibu wao isije ikawa kuna kasoro iliyofichika au makosa... Hii ndio Taqwa.

Kwa kifupi hawa ndio waaminio ambao hawana kujiachia huria katika mambo yao, iwe yanamhusu Mwenyezi Mungu au yanawahusu watu. Kwa kweli kwa sababu ya hofu kwamba wasije wakawa ni wenye kulaumiwa mbele ya macho ya Allah Mwenye Enzi, wanachukua tahadhari kubwa sana juu ya amana na ahadi zao. Wanatafakari wakati wote juu ya amana na ahadi zao na mara kwa mara wanazikagua hali zao za ndani kwa kuitazama kila chembe kwa Taqwa kwa kuhofu kwamba isije kukawa na kasoro iliyofichika katika kutimiza kwao dhamana na ahadi. Wanazitumia amana walizopewa na Allah Mwenye Enzi, kwa mfano vipaji vyao vyote, viungo vyao, uhai, mali na heshima n.k kwa kadiri ya uwezo wao, ndani ya mipaka ya Taqwa na kwa uangalifu na kwa wakati muafaka. Utendaji wao unakuwa daima ni kwa uaminifu wa hali ya juu kabisa na kwa kadiri inavyowezekana hujaribu kuitimiza ahadi waliyofunga na Mungu Mwenye Enzi wakati walipoikubali imani. Vile vile, kadri wawezavyo, wanatimiza kwa Taqwa amana za watu walizo nazo au ambazo zitahitaji kutekelezwa chini ya dhamana walizopewa. Kukiweko na mzozo, wanautatua kwa kushika msingi wa Taqwa, hata pale hukumu itakapowadhuru wao wenyewe.’ (imefasiriwa kutoka Tafseer of the Holy Qur’an by the Promised Messiah (a.s), Vol III, pp 366 – 367).

‘Uzuri wa kiroho wa mtu ni kutembea katika njia nyembamba za Taqwa. Hizo ndizo alama za kuvutia za uzuri wa kiroho. Ni dhahiri kwamba kuwa mwangalifu na amana za Mwenyezi Mungu, na kutimiza ahadi zote za imani, na kutumia vipaji na viungo vilivyo dhahiri na vilivyofichika kama akili na vipaji vingine, katika wakati wake muafaka na kuvizuia visitumike isivyofaa, na kushika hadhari dhidi ya mashambulizi ya siri siri ya shetani na kuzingatia haki za viumbe wenzake, ndio moja ya kukamilisha haiba ya kiroho ya mtu. Mungu Mwenye Enzi ndani ya Qur’an ameifananisha Taqwa na nguo. ‘Libas ut taqwa’ ni usemi wa Qur’an Tukufu. Hii inaonyesha kwamba uzuri wa kiroho na mapambo ya kiroho yanapatikana kwa Taqwa. Taqwa maana yake ni kwamba mtu anapaswa kuangalia hata nukta ndogo ndogo kabisa za amana za Mwenyezi Mungu na ahadi na hali kadhalika amana na ahadi zote za viumbe wenzake, kwa kadri itavyokuwa inawezekana. Ndio kusema, mtu ni lazima ajaribu kutimiza kwa kadri ya uwezo wake, wajibu wake wote bila kuacha hata chembe ndogo.’ [Brahin-e- Ahmadiyya, Part V, Ruhani Khaza’in, vol.21, pp. 209-210 – Essence of Islam, Vol.1.pp 347 - 348].

Bila kiwango cha Taqwa kuwa juu haki za amana na ahadi kwa Mwenyei Mungu na kwa wanadamu haziwezi kutimizwa. Viongozi wanachukuliwa kimaalum kama wabebaji wa dhamana za haki zote hizi mbili. Hadhrat Khalifatul Masih akazielekeza tena fikra za Wanajumuia katika kufanya maombi kuwachagua wale ambao huzitimiza ahadi zao. Ili kufanikisha hili kila mmoja ni lazima awe na kiwango cha juu kabisa cha Taqwa kila mmoja anahitaji kujichunguza na kupandisha kiwango chake cha Taqwa. Viongozi wanachaguliwa na wanajumuia kutokana na wanajumuia. Hapa chini zipo sifa ambazo viongozi kimahsusi na waaminio kwa ujumla wanahitajika kuwa nazo:

Kutimiza ahadi: Ikiwa kiwango cha kutiza ahadi ni cha juu ndani ya Jumuiya, kitakuwa cha juu pia kwa viongozi. Haki haitendeki pale ambapo ahadi haziheshimiwi. Masih Aliyeahidiwa (a.s) ametufundisha kwamba haki za wengine ni lazima zitolewe hata kama itatulazimu kutaabika kwa ajili ya hilo. Islam ni dini ya amani na ingawa inatilia mkazo mkubwa katika njia zenye kulinda amani, uvunjaji wa ahadi umeenea na misuguano imeenea kati ya Waislam. Jambo hili lina athari kwetu wanajumuia pia. Ahadi ambazo zinahitaji kutekelezwa na kuheshimiwa sio mikataba ya kibiashara peke yake. Bali ndoa pia ni mkataba lakini watu wanadanganyana juu ya mambo ya majumbani mwao. Hadhrat Khalifatul Masih akasema kwamba amewahi kulitaja jambo hili kabla kwamba wapo watu ambao wanatimiza wajibu wao katika Jumuiya vizuri lakini hawatimizi majukumu yao ya kifamilia. Huku ni kuvunja makubaliano na kunastahili adhabu mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu. Anasema: ‘… na watekelezao ahadi zao wanapoahidi...’ (2:178). Ikiwa waahmaadiyya wanataka kuwachagua viongozi wacha Mungu wanatakiwa waangalie ni kwa kiasi gani watu husika wanatekeleza ahadi zao binafsi.

Imeelezwa pia kwamba kwa ajili ya kuunda jamii yenye amani tuzijali hisia za wengine. Imesemwa: ‘… Wala msiwasingizie watu wenu wenyewe, wala msitushane kwa majina mabaya...’ (49:12). Neno la Kiarabu lililotumika katika aya hii lina maana pana zaidi. Linamaanisha pia kusukuma kando, kutafuta makosa ya wengine, au kusema jambo linaloumiza. Tunaona kwamba wakati mwingine viongozi hawazizuii hasira zao na kuumiza hisia za wale wanaowatumikia na wakati mwingine za viongozi wenzao. Inatokea kwamba wale wenye imani dhaifu wanagombana na viongozi kama hao na wakati mwingine wanajenga chuki dhidi ya Jumuiya. Aya inaonya pia dhidi ya kuwadhihaki watu kwa majina wasiyoyapenda na kumtendea kila mmoja kwa heshima. Hii ni sifa adhimu ambayo viongozi wanapaswa kuwa nayo. Ingawa kila mwaminio anapaswa kuzingatia sifa hizi viongozi wanatakiwa kuwa na uangalifu maalum.

Sifa nyingine inayotakiwa kwa viongozi wa Jumuiya ni kutumia fedha za Jumuia kwa uangalifu mkubwa. Kwa

Endelea uk. 5

Msikiti mwingine wafunguliwa Valencia

Kutoka uk. 2

majirani wema kwa fadhili za Mwenyezi Mungu. Haitakiwi tu tusifie na kufurahia kujenga msikiti mzuri katika mji mwingine wa Uhispania. Tunatakiwa tujichunguze, tuongeze viwango vyetu vya ibada na kila mmoja wetu ajitahidi kutekeleza majukumu yake.

Aya za Quran Tukufu zilizosomwa mwanzoni zinaeleza vyema jinsi Hadhrat Ibrahim na mwanawe Hadhrat Ismail a.s. walivyotufundisha namnayakutekelezamajukumu yetu sambamba na ujenzi wa nyumba za Mungu - misikiti. Tunalazimika kulizingatia sana jambo hili ili katika vizazi vyetu vijavyo wapatikane watu watakaoendelea kuheshimu haki na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Aya hizi zinayo maombi ambayo Hadhrat Ibrahim aliyaomba wakati alipokuwa akiinua kuta za Ka'ba. Baada ya miaka kadhaa ya kujitolea muhanga kwa baba, mama na mtoto, Mwenyezi Mungu hakuyafanya maombi yao yapotee bure. Huu si utamaduni wa Jamaat Ahmadiyya bali waislamu wengine hujisifia kwa hata kujitolea kidogo kunakofanywa.

Mfano ambao Mwenyezi Mungu ametuonyesha kwa Mitume wake hawa ni kwamba: Pamoja na kuwa baba alijitolea muhanga na akawa tayari kumtoa dhabibu mtoto wake aliyempata katika umri wa uzee, lakini na mtoto naye akawa tayari kukubali kutolewa kwake dhabibu. Pia akawatoa muhanga mke na mtoto wake kwa kuwaacha jangwani ambapo hapakuwa na chochote. Na kujitolea kwao kukubaliwa na Mwenyezi Mungu na akawabariki sana. Wakati waliinua kuta za kaaba watu hawa wawili wakatangaza kwamba lengo lao sio jingine zaidi ya kuifanya nyumba ya Mwenyezi Mungu ifikiwe na watu na sio ifikiwe na watu wa kawaida tu, bali ifikiwe na waumini watakaojali wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu na watakaojitahidi kufikia viwango vya juu vya uchamungu. Watu hawa walijenga nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa amri Yake licha ya unyenyekevu na mapenzi yao kwa Mwenyezi Mungu bado walimuomba akubali kujitolea kwao. Hili ndilo somo la kujitolea; mtu ajitolee muhanga na kisha amgeukie Mwenyezi Mungu kwa moyo na unyenyekevu wote akimuomba akubali kujitolea kwake alikukofanya. Ni mtazamo huu wa Kiibrahim na Kiismaili ndio unaotakiwa uamshe tafakuri zetu kwamba sisi ni wafuasi wa yule mtu ambaye – kutokana na mapenzi yake na kujitolea kwake kwa Mtume s.a.w. – alipewa lakabu ya Ibrahimu wa zama hizi na Mwenyezi Mungu mwenyewe. Mtu huyu ameziinua tena kuta za jengo la Islam lililokuwa limeporomoka na akaung'arisha uso mzuri



Masjid Basharat, Pedroadbad Uhispania. Msikiti wa kwanza kujengwa nchini humo baada ya karne 7 za maanguko ya Uislamu barani Ulaya

wa Islam na akauwasilisha mbele ya dunia kwa utukufu wake kamili, kiasi hiki kwamba hata wasiokuwa waislamu wanasema ikiwa huu ndio Uislamu basi tunafuta tuhuma zetu zote tulizousingizia Uislamu.

Leo malengo yale ya kujengwa kwa Kaaba yanatimizwa vizuri na Ibrahim huyu na nuru ya mafundisho mazuri ya Islam inawekwa bayana mbele ya dunia. Kila msikiti wetu unaojengwa duniani ni shahidi wa kutimizwa kwa malengo haya na msikiti wetu huu uliopewa jina la Baitur Rahman pia nao ni kielelezo cha kufikiwa kwa malengo hayo hayo. Wakati ambapo msikiti huu unatukumbusha kugeukia kwa unyenyekevu kwenye malengo yetu, pia unatukumbusha kujali viapo vyetu na kutekeleza majukumu yetu. Ni hapo tu ndipo tutakapoweza kufikia malengo yetu.

Tunasema "Ewe Masihi wa Muhammad, ewe mpenzi na mtumishi wa kweli wa Mtukufu Mtume s.a.w. tumechukua kwako kiapo cha utii kwamba tutatanguliza matakwa ya imani mbele kuliko yale ya kidunia na tutatangaza Tawhed (Umoja wa Mwenyezi Mungu). Ujenzi wa msikiti huu utakuwa ni njia ya kuikumbusha dunia juu ya Islamu na kufunguka kwa njia mpya za kimahubiri. Kwa kutimiza mahitaji yake kwa kutumia vipawa vyetu, vyote jukumu letu la mwanzo litakuwa ni kuimarisha tawheed na kuwarudisha tena watu wa nchi hii kwenye bendera ya Mtukufu Mtume s.a.w. E Mwenyezi Mungu mwenye kusikia na Mjuzi wa yote yasikilize maombi yetu na tuwezeshe kutimiza majukumu yetu. Ufanye msikiti huo kuwa sababu ya kufikiwa kwa malengo hayo, ambayo ndio malengo ya kujengwa kwa nyumba zako. Wewe ni Mjuzi wa yote, unaujua udhaifu wetu, tukubalie maombi yetu, na utughufirie, na utuwezeshe kufikia malengo yetu."Amin.

Kwa hakika uzuri na umuhimu wa msikiti unaweza tu kuonekana iwapo tutatimiza wajibu wetu, pale ambapo tutatimiza haki/amri za Mwenyezi Mungu na pia tutatimiza haki za viumbe wa Mwenyezi Mungu kiasi hiki kwamba mfano halisi wa mafundisho ya islam uonekane kwa vitendo na watu wavutike nao.

Katika kipindi cha utawala wa miaka mingi wa Waislamu hapa Uhispania, misikiti mingi na mizuri sana ilijengwa. Mfano, msikiti wa Cordoba, uzuri wake unawashangaza wengi hadi leo. Pia iko misikiti mingi ambayo ilijengwa kila waislamu walipokwenda. Kuna msikiti mwingine uko Granada. Hata hivyo, zama ambapo mafundisho ya kweli ya islam yalitoweka kwenye nyoyo za waliokuwa wakiitumia misikiti hii, basi hapo majengo haya ambayo mwanzoni yalikuwa yakitangaza Umoja wa Mungu, ama yalibomolewa au yalibadilishwa kuwa makanisa. Mtu anashangazwa na uzuri na uimara wa Msikiti wa Cordoba ambao umebaki bila kubadilishwa kwa karne nyingi, lakini kwa bahati mbaya msikiti huu ukafanywa kuwa kanisa. Wakati waislamu walipopoteza roho ya imani zao, misikiti yao pia ikaenda kwa wengine. Hivyo jambo kubwa sio ukubwa au uimara wa jengo la msikiti. Jambo kubwa zaidi ni kiwango cha imani cha wale wanaoijaza misikiti hiyo. Hivyo, tunatakiwa tuendeleze roho ya msikiti huu kwa kufanya juhudi na pia kwa maombi ili Mwenyezi Mungu aendelee kuinuwa watu miongoni mwetu watakaokuza moyo huu ili kwamba msikiti huu uendelee kuwa ni kituo cha Tawhed hadi siku ya mwisho.

Katika aya ya pili iliyosomwa mwanzoni, manabii hawa watukufu hawakuishia maombi yao kwao tu bali walipanua wigo wa maombi yao kwa vizazi vyao vijavyo. Hii kwa hakika ndio njia ya maombi, na shauku ya wale wanaotaka mafanikio kwa vizazi vyao vijavyo na vijavyo. Hivyo, InshAllah tutakuwa wenye kufanikiwa na kwa maombi yetu kwamba na vizazi vyetu pia vishikamane na taqwa tunaweza kufikia malengo ya kujengwa kwa nyumba za Mwenyezi Mungu. Kujitolea kwetu kutakubaliwa tu iwapo tutaendelea kuwa na watu watakaojali wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu na watakaojali wajibu wao kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu. Tunalazimika kumuomba Mwenyezi Mungu kama walivyoomba Manabii hawa 'Na Utuonyeshe njia za ibada yetu'. Kwa hakika njia za ibada na kujitolea zinaeleweka kwa kuongozwa na Mwenyezi Mungu. Uwezo wa kuzielewa kwa undani unaweza kufikiwa tu kwa rehema za Mwenyezi Mungu. Sala bila shaka ni moja ya njia za ibada. Lakini wapo ambao Mwenyezi Mungu anasema sala zao zitawarudia wenyewe na kuwa sababu ya maangamizo yao. Mtu anatakiwa ajitahidi kusimamisha sala yake kwa kiwango ambacho itakubaliwa na Mwenyezi Mungu kwa rehema zake. Kwa hali hiyo chochote kifanywacho katika njia yake kinakuwa ni aina ya ibada, hata kuwatumikia binadamu.

Tukiombee sana kizazi chetu. Tunaahidi katika kila kikao kwamba tutakuwa tayari kujitolea mhanga, basi tujenge pia dhamira hii kwa vizazi vyetu. Hata hivyo, inabidi tuelewe kwamba aina ya kujitolea inaweza kubadilika sawa na mazingira. Waislamu wa mwanzo walipokuja Uhispania kuueneza Islam iliwabidi wapigane jihadi ya upanga. Hata hivyo, jihadi ya leo hasa ni tabligh na kujitolea mali zetu kwa ajili ya ujenzi wa misikiti. Aina ya kujitolea inabadilika sawa na wakati. Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) aliomba kwa Mwenyezi Mungu kwamba aelimishwe juu ya njia za kujitolea na kwa njia hiyo akatupatia mwongozo kwamba kimsingi aina ya kujitolea inaweza kubadilika sawa na mazingira.

Wema unatakiwa utimizwe ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Hii ndio maana Mtukufu Mtume s.a.w. katika mazingira fulani alisisitiza kuswali tahajjud kuwa ni wema mkubwa zaidi na katika mazingira mengine akasema wema zaidi ni kufanya jihadi. Hivyo wema tuukosao kwa wakati fulani basi huo unakuwa ndio wema mkuu kwa wakati huo na huo pia unakuwa ndio ibada muhimu zaidi kwetu na hiyo pia inakuwa ndio njia kuu ya kujitolea kwa ajili yetu. Dua hii inatusisitizia sana kujitahidi kuondoa udhaifu wetu na wa vizazi vyetu. Na pia ikumbukwe kwamba viwango vya juu vya ibada haviwezi kufikiwa kwa juhudi tu pekee wala kwa kujitolea tu. Na hii ndio sababu tunatakiwa pia tuombe "na Utuelekee kwa rehema" ili kwamba kujitolea kuzalishe kujitolea kwingine na kuabudu kuwe ndio msingi mkuu wa mawazo yetu.

Bahati ni kwa wale ambao watafuata njia hii na wataingia katika hifadhi ya Mwenyezi Mungu kutokana na udhaifu na dhambi na pia wakawaombea vizazi vyao na kuwajengea msingi huu. Tunatakiwa tukumbuke kutekeleza haki ya viumbe na kuepuka makuu na majivuno. Tuondokane na uvivu wa kusali, na Sala yoyote inayoonekana ngumu kwetu tunatakiwa tusali kwa umakini na uangalifu zaidi. Kama kusali Sala za jamaa ndio udhaifu wetu, tunatakiwa tujitahidi kukabiliana na hilo. Kama hatuheshimu haki za wazazi wetu, tunatakiwa tuziheshimu, kama hatutimizi haki za watoto, tunatakiwa tuzingatie hilo. Kama hatuheshimu haki za jirani zetu tunatakiwa tuzingatie hilo na kuwavutia kwenye Ahmadiyyat, Uislamu wa kweli. Kama tunatekeleza wema wote huu basi hapo ndipo tutakapoweza kumwomba Mwenyezi Mungu kikwelikweli atukubalie toba yetu na kuturehemu. Hakika tunatakiwa tuwatendee wengine kwa huruma ikiwa tunataka Mwenyezi Mungu atuhurumie.

Mwaminio anapojikita msikitini, milango mipya ya wema hufunguka na husamehewa. Leo msikiti huu tuliojaaliwa na Mwenyezi Mungu unatakiwa utukumbushe kutafuta neema hizi. Wale wanaoishi katika eneo hili wanatakiwa kuujaza msikiti huu, pia wafike na watoto wao msikitini kufanya ibada, InshaAllah. Mwenyezi Mungu awajaalie Baraka zote ambazo zinatokana na msikiti huu na Apokee toba na Asamehe upungufu uliopo! Leo tunatakiwa kufanya Jihadi ya nafsi. Kueneza ujumbe wa Islam pia ni Jihadi na tunatakiwa tuzingatie hilo. Hatuwezi kufanikiwa pasipo msaada wa Mwenyezi Mungu. Rehema ya Mwenyezi Mungu inapatikana kwa kutimiza haki za ibada zake. Tutapata Baraka zake kwa kutekeleza Sala na kushiriki katika Jihadi ya nafsi na Jihadi ya kueneza ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Jamii ya leo inamhitaji sana mwanadamu katika Jihadi hii. Jihadi hii pekee ndio itakayotuokoa na uovu uliopo katika jamii na kutufanya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kutuokoa sisi pamoja na kizazi chetu dhidi ya uovu wa dunia. Upambeni msikiti huu kwa ibada ya kweli. Mwenyezi Mungu Aufanye msikiti huu utimize malengo, nasi pia atuwezeshe kutimiza majukumu yetu. Tayari msikiti uliofadhiliwa na chi za Misri na Saudi Arabia umejengwa katika jimbo hili. Kile kinachokosekana (kwenye msikiti huu) kutokana na wao kutomkubali Masihi wa Muhammad (Saw) kinaweza tu kupatikana kwenye msikiti wa Ahmadiyya. Ukweli huu unatakiwa umkumbushe kila Muahmadiyya kuhusu kuongezeka kwa majukumu yetu. Mwenyezi Mungu atuwezeshe kutimiza hili. Amin.

Kuhusu takwimu za msikiti huu, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema kuwa umejengwa katika kiwanja chenye fiti za mraba 1,350 kwa gharama ya Euro milioni 2.1 (sawa na shilingi za Tanzania takriban bilioni 2.5) ambapo Jamaat ya Uhispania imechangia kiasi kidogo. Kama kuna uhaba wa fedha, tutashukuru kuendelea kupokea ahadi za michango, lakini njia nyingine ya kuchangia ni kushiriki katika mpango wa Tabligh. Imeelezwa kuwa ukumbi huu unaweza kuchukua watu wapatao 250, lakini kumbi ni kubwa zaidi. Viambajengo vingine ni pamoja na ofisi saba, maktaba, duka la

Endelea uk. 5

Mungu Ibariki Kenya, Ibariki

Kutoka uk. 1

kwa Rais mpya, amekubali maamuzi yote yaliyofanya na vyombo halali katika kufikia maamuzi ya kuthibitisha matokeo ya uchaguzi huo, kubwa zaidi alionekana runingani akiwa Ikulu ya Kenya na Rais mpya wakicheka na kutaniana jambo ambalo linaonyesha wamekubaliana kujenga Kenya imara zaidi. Sisi katika Afrika ya Mashariki tuna matumaini makubwa na mshikamano ule na tunaomba uwe kwenye mioyo yao na siyo ya kinafiki. Afrika inawategemea viongozi hawa wa Serikali na upinzani kuwa kitu kimoja na kuzika tofauti zao za awali kwa dhati.

Katika kufikia malengo ya Serikali mpya, tunaamini Rais mpya wa Kenya atavunja makundi yaliyokuwepo kabla ya uchaguzi, atawaunganisha wakenya wenye maradhi ya ukabila, ataondoa makovu ya uhasama, chuki na visasi, atajiepusha na kupigana vijembe vya kisiasa pasipo na ulazima. Katika kufikia hilo linahitaji dhamira ya kweli ya siasa za kizalendo, na siyo siasa za kutumiwa na watu kulipa fadhila ya pale ambapo Mheshimiwa Uhuru Kenyata amefika. Ushindi wa Uhuru Kenyata uchukuliwe kuwa ni ushindi wa Wakenya wote na kutambua kuwa lipo kundi kubwa la Wakenya kwa sababu za kidemokrasia hawakutaka Mheshimiwa Uhuru Kenyata awe Rais wao, hawa pia wanapaswa kuheshimiwa na kuthaminiwa kwa uamuzi wao huo, siyo kutengwa, kuhujumiwa na kupigwa vijembe ili wajutie uamuzi wao huo. Harakati za namna hii huwa hazina mwisho mzuri kwa Serikali yeyote ile, zinajenga usugu, chuki na udumaza demokrasia na kuiweka rehani amani ya nchi. Katika Taifa kama la Kenya lililopita katika msukosuko mkubwa wa mauaji mambo haya hayapaswi kupewa nafasi hata kidogo.

Dunia inatambua kuwa Mheshimiwa Rais ni Mshitakiwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Uholanzi The Hague juu ya kadhia ya mauaji yaliyopita nchini Kenya. Ni juu ya wakenya wote kuomba Mungu haki itendeke kwa Rais huyu na katika hili tunapaswa kuiachia Mahakama ifanye maamuzi, kama tulivyoacha Mahakama iamue juu ya hatima ya uchaguzi wa Kenya. Sasa Wakenya wamehitimu mafunzo ya kusubiri na kuheshimu maamuzi Mahakama, tunaamini watashinda mtihani huu wa kuvumilia pale wanapoona Mheshimiwa Rais anapanda kizimbani.



Picha ya zamani: Je kilikuwa ni kikao cha upangaji safu ya Uongozi Kenya ?

Mheshimiwa Rais ni mtoto wa muasisi wa Taifa la Kenya, Jomo Kenyata, ambaye kwa muda mrefu alikuwa anamfundisha siasa mtu ambaye alikuja kuwa mrithi wake, huyu ni Daniel Arap Moi na wakati fulani Jomo Kenyata wakati wa utawala wake aliwahi kuwa nao katika kazi zake za kila siku pamoja na Mwai Kibaki. Katika kipindi hiki Mheshimiwa Rais alikuwa ni mdogo lakini atakuwa anakumbuka namna Jomo Kenyata ambaye ni baba yake alivyowasaidia katika kufikia malengo yao ya kisiasa. Alipofariki Jomo Kenyata mnamo 1978, nafasi yake ilichukuliwa na Mzee Daniel Arap Moi hadi 2002 ambapo Mzee Moi alimpendekeza Uhuru Kenyata awe mgombea wa Urais. Katika uchaguzi huo Mheshimiwa Uhuru Kenyata alikuwa na miaka 41 alishindwa kwa sababu wakenya walijua fika kuwa lilikuwa ni chaguo la Mzee Moi hivyo angemburuza katika kuendesha nchi. Wakati watu wa Kenya wanamuadhibu Uhuru Kenyata, wanampatia nafasi hiyo mfuasi mwingine wa damu wa Mzee Jomo Kenyata aliyejiondoa KANU ili kufikia malengo ya kisiasa, huyu ni Mzee Mwai Kibaki. Kwa maana hiyo nafasi hii haikwenda mbali na Mheshimiwa Uhuru Kenyata akafanya maandalizi kamambe ya kuingia Ikulu kwa msaada wa watu wengi wakiwemo hawa waliofanya kazi na baba yake. Hatimaye Mheshimiwa Uhuru Kenyata amekuwa Rais wa nne wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa Kenya. Tarehe 4 April 2013, Mheshimiwa Rais mteule alimtembelea Mzee Moi nyumbani kwake Nairobi kwa kile kinachoelezwa kutoa shukrani na mazungumzo ya kina juu ya masuala ya Serikali atakayoiunda.

Huu ni mwisho wa mwanzo wa safari ndefu ambayo watu wa Kenya wanatakiwa kufanya kwa Serikali yao itakayoundwa, kubwa kutoa ushirikiano ili kujenga Kenya moja isiyo na ukabila na yenye amani tele. Mungu Ibariki Kenya, Ibariki Afrika ya Mashariki, Ibariki Afrika yote.

'Uongozi ni dhamana' - Khalifa Mtukufu

Kutoka uk. 3

hali yoyote ile kusiwepo na ubadhirifu. Ingawa idara zenye matumizi makubwa, kama Ziafat, Langar, Jalsa Salana zinazo pia bajeti kubwa lakini wasimamizi wa idara hizo hawana budi kuwa waangalifu sana. Makadirio yanatakiwa yafanyike na gharama za chini zaidi zifanyike. Hii ndio namna sahihi ya kutimiza ahadi. Masih Aliyeahidiwa (a.s) hakuwahi kuwa na shaka juu ya upatikanaji wa fedha bali shaka yake ilikuwa juu ya watu kuzitumia fedha ipasavyo.

Sifa nyingine ya kiongozi ni kwamba anatakiwa kujiepusha na yale yote ambayo ni upuuzi na yasiyo na maana. Kwa hakika hii ni alama ya kila Mwaminio lakini wale waliokabidhiwa majukumu ya Jumuiya wanapaswa kuwa mfano halisi wa hili. Mwenyezi Mungu anasema: 'Na ambao katika upuuzi ni wajiepushao' (23:4). Kiwango cha ubora miongoni mwa waaminio juu ya hili kinatakiwa kuwa cha juu sana. Hawatakiwi kujumuika katika maongezi ya mizaha na hawatakiwi kuwepo katika mikusanyiko ambamo kuna kejeli na utovu wa heshima dhidi ya wengine. Wakati mwingine watumishi huwa wanakaa pamoja na kuwaongelea wengine kwa kejeli. Hili lapaswa kuepukwa. Watumishi hawatakiwi pia kuwapo kwenye mikusanyiko ambamo desturi za kidini zinadharauliwa.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema kwamba mwaminio ni yule ambae anajiondoa kutoka kwenye mahusiano yasiyo na maana na yasiyofaa; kujiondoa kutoka kwenye mahusiano yasiyo na maana na yasiyo faa ni chanzo cha kuunga mahusiano na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, kuyaondoa mambo yasiyo na maana kwenye moyo wa mtu ni kuunga moyo wa mtu na Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu anasema bahili hawezi akawa Mwaminio. Viongozi inawabidi waepuke ufujaji na wawe na kiasi katika matumizi, lakini wasiwe wabahili pia. Mtu anapaswa kufanya matumizi kila pawapo na haja. Haitakiwi kwamba mtu anakuwa mkarimu kwa baadhi ya watu na bahili kwa wengine.

Sifa maalum ya watumishi inayotakiwa ni kwamba wawe na uwezo wa kutawala hasira zao. Inasemwa: '… na wanazuia ghadhabu...' (3:135). Wakati mwingine chukizo lapaswa kuelezwa kwa nia ya kurekebisha watu katika nidhamu ya Jumuia lakini viongozi wanatakiwa kuweza kuzuia ghadhabu zao. Ni jambo lisilokubalika kwa viongozi kukasirishwa na kila jambo dogo. Wanapaswa kuzingatia kwamba Qur'an inasema '… na semeni na watu kwa wema...' (2:84). Ikiwa hili litafuatwa watu wataacha kutoa malalamiko dhidi ya viongozi.

Viongozi wanatakiwa kuwatendea watumishi wenzao kwa wema. Mahusiano hayapaswi kuwa kama yanayokuwapo baina ya bosi wa kidunia na wachini zake. Ikiwa mtu amefanya kosa fulani aelekezwe kwa upole na hakutakiwi kuwepo na mahojiano kama yale ya mabosi wa kidunia. Kwa hakika, kama mtu hafuati utaratibu, hilo linapaswa kushughulikiwa na haja ikiwepo liripotiwe. Hata hivyo, kusiwepo na hali inayoweza kupelekea kuleta migawanyiko.

Viongozi wanatakiwa kuwa na sifa ya kuwakaribisha wageni. Mtu yeyote anayekuja Ofisini akaribishwe kwa heshima na kupewa kiti; hili ni jambo la muhimu sana. Mtu anatakiwa asimame kuwasalimia. Bashasha ya namna hii inatakiwa ifuatwe na viongozi wa kuchaguliwa na watumishi wengine wote wa kawaida wa Jumuiya. Hii inakuza na sio kupunguza heshima.

Upole ni sifa ambayo kila Ahmadiyya anapaswa kujijengea, hususan viongozi. Imesemwa: 'Wala usitembee katika ardhi kwa maringo...' (17:38). Mungu hapendi majivuno kwa watu wa kawaida. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu hatapenda hata maringo ya mpito tu kwa wale wanaotoa huduma zao kwa ajili Yake. Sifa hii ishikiliwe na viongozi wetu wote kwa ukamilifu kabisa.

Jambo jingine la muhimu hasa kwa wale waliopewa majukumu kuhusiana na kufanya maamuzi na usuluhishi, kama vile Kamati ya Islahi au Bodi ya kadha, ni kuwa waangalifu kwa kushika amri ya Mwenyezi Mungu: '… shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa...' (5:9). Kila uamuzi uwe kwa msingi wa usawa na haki. Wakati mwingine maamauzi yaliyofanyika anafikishiwa Hadhrat Khalifatul Masih ambayo hayakuangalia vyema kuhusiana na matokeo yatakayoletwa nayo na kwa ajili hii watu wanapata mashaka. Ikiwa maamuzi yamefanyika kwa msingi wa Sharia basi hapo na ielezwe wazi. Makadhi wanatakiwa kuwa waangalifu hasa juu ya jambo hili.

Kila panapokuwa na watu wahitaji na maskini, wanatakiwa waangaliwe na Jama't. Ni jukumu la maAmir husika na viongozi kuwahudumia sawa na raslimali iliyopo. Kwa hali hii matendo hayana ulazima wa kusubiri mpaka maombi yatolewe. Kinyume chake hali inapaswa kutathminiwa kila wakati.

Wajibu mkubwa unaoangukia kwa kila Ameer, kila Sadr na kila kiongozi ni: '… mnaamuru yaliyo mema na mnakataza maovu...' (3:111). Hili lapaswa kuzingatiwa wakati wote. Bila shaka inawezekana tu kushikamana na hili pale ambapo; mtu anajikagua na kufanya neno lake na matendo yake kufanana, atatia moyoni mwake mapenzi na hofu ya Mwenyezi Mungu na kutafuta njia za Taqwa ambazo Mwenyezi Mungu ametuelekeza. Masih Aliyeahidiwa (a.s) aliwahi kusema kuhusiana na hili kwamba Taqwa sio kuacha madhambi fulani na kutenda mema fulani. Bali, Taqwa maana yake ni kuepuka kila dhambi hata ndogo na kufanya kila aina ya wema.

Katika kuhitimisha Hadhrat Khalifatul Masih alisema: 'Hivi ndivyo viwango tunavyohitaji kuvifikia sisi sote ili tuwe ni wale wanaoamrisha mema na kukataza maovu na tuweze kutimiza ahadi zetu. Allah Mwenye Enzi na Awawezeshe wanajumuia na hali kadhalika viongozi, wale waliochaguliwa na wale watakaochaguliwa, na mimi kutimiza dhamana zetu na ahadi zetu'.

Msikiti Valencia

Kutoka uk. 4

vitabu, jiko maridhawa, stoo na chumba cha ufundi. Jengo hili lina kiyoyozi. Ingawa tayari eneo hili lilikuwa na mahali pa makazi, vyumba vitatu zaidi vimeongezwa. Magazeti yameripoti kwamba jengo kubwa kwa ajili ya ibada jimboni limepatikana. Hata hivyo, kupatikana kwa jengo hili (msikiti) kutakuwa na maana iwapo kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake. Jambo jingine zuri lililotajwa katika magazeti ni kwamba kutokana na kujitolea kwa waahmadiyya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wanapinga wale wote wanaofanya mauaji kwa kutumia jina la Mawenyezi Mungu. Aidha, msikiti una kumbi mbili kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Mwenyezi Mungu ajaalie msikiti huu uwe kielelezo cha picha ya kweli ya Islamu kwa watu wa eneo la jimbo hili na ajaalie kila Muahmadiyya atimize majukumu yake.

Msaada mkubwa kwa ajili ya ujenzi wa msikiti huu umetoka Markazi. Aidha, msaada wa kiufundi umetoka Markazi. Mhandisi wetu mkongwe, Chaundry Ijaz Sahib aliratibu kazi mbalimbali pamoja na kufanya upembuzi yakinifu. Alipunguza gharama pale zilipokuwa juu mno lakini bila kuathiri viwango vya ubora wa jengo. Hali yake ya afya si njema sana na anapata matibabu ya figo kila wiki lakini anajitahidi sana. Mwenyezi Mungu Amlipe malipo mema na Amjaalie afya njema ili aweze kuendelea kuitumikia Jamaat. Amin.

Bustani ya Washairi

Maradhi hatari ya 'shirk' yameshamiri sana katika kutafuta watoto, mali na mapenzi. Binadamu yuko tayari kutumia mbinu zote anazozifahamu akijidanganya kwamba atapata vitu hivyo tulivyovitaja hapo juu bila ya mapenzi yake Mwenyezi Mungu. Mmoja wa Washairi maarufu nchini Sihiyana Swaleh Omari Muhanuka maarufu kama Mandevu Mtenda mema, ametuonya juu ya upuuzi wa kutumia dawa ili kupalilia mapenzi. Amesema hiyo ni shirk na upuuzi. Yeye anasisitiza ya kwamba mapenzi hayana dawa linalotakiwa ni kumuomba Mwenyezi Mungu awaimarishe nyote:-

1 Mapenzi hayana dawa, walisema watanguzi
Bure tunajisumbuwa, kuchimbachimba mizizi
Pesa zetu zinaliwa, na waganga wanyakuzi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

2 Penzi mfano wa mvuwa, masika na kiangazi
Mimea ikichipuwa, inahitaji palizi
Miche ipate kukuwa, uvune kiwe kizazi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

3 Mapenzi yakishamiri, huwa mithili ya chizi
Hata noti huzijali, waona ganda la ndizi
Si mchana si laili, wewe huna usingizi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

4 Na yule anayependwa, huonekana ana enzi
Kila aendapo hulindwa, kama polisi na mwizi
Alalapo anakandwa, hata kufa hakuwazi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

5 Mwisho penzi husimama, hakutaki kijakazi
Huporomoka milima, kutafuta waganguzi
Nipe dawa himahima, mwenzio nina malazi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

6 Mganga hapo hucheka, akarudisha pumzi
Riziki ishanifika, kuiachia siwezi
Shilingi mia haraka, toa niianze kazi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

7 Husema kalete njiwa, kuku mweupe na mbuzi
Vipande saba vya miwa, zafarani na kunazi
Mkame bata maziwa, na pangaa za viazi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

8 Lete shuka doti mbili, na manyoyo ya papazi
Tafuta panya wawili, mmoja achunwe ngozi

Weka kwenye makaburi, usiku wa mbaramwezi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

9 Nitakupa mkataba, ukifanya dawa hizi
Haifiki siku saba, atafika kama njozi
Mimi sipendi ghiliba, ni mganga wa kikozi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

10 Ndugu nawafahamisha, hayana dawa mapenzi
Bure kujishughulisha, gharama hizi na hizi
Yakiisha yamekwisha, imebaki simulizi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

11 Kaditama ndiyo mimi, papa mzamia mbizi
Sijisifii kwa ngumi, wala vichwa sivi wezi
Ila vita ya ulimi, tutaimaliza miezi
Mapenzi hayana dawa ila masikilizano.

Kwa kuitikia wito wa Mtukufu mtume Muhamamd s.a.w. kwamba asiyeoa si miongoni mwetu, mwl. Twaha Nyange alipeleka maombi yake kwa Allah ili apate mke mwema:

NDOANIKITUAULA,MWENZENUNIMEZAWIJI.

1. Bismillahi Jalali, ni yeye ndiye Mpweke
Kapwekeka kila hali, misada yatoka kwake
Hatokezei wa pili, wa kutenda kazi zake
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

2. Mpokezi wa maombi, anapoombwa kwa dhati
Khasa ukiacha dhambi, hakuambii hupati
Hakupigii firimbi, kwamba umezidi goti.
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

3. Nilipeleka maombi, kwake Mola maulana
Anipambe kwa kitambi, kwa libasi yenye jina
Isokuwa na vitimbi, moyo wangu ukachana
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

4. Maombi ya mke mwema, nilikuwa nayo toka
Bado ningali nasoma, kule Pugu nakumbuka
Kila niliposimama, kwa swala nikitamka
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

5. Nilimwambia Rabana, yangu yaletayo dhwila
Kwamba anipe kimwana, mshika dini ya Mola
Asiwe mshirikina, wala shaghala baghala
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

6. Nilifunga na swaumu, na swadaka kama chambi
Na usiku wa naimu, naamka kwa maombi
Nafali nikiikimu, ambayo haina kimbi
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

7. Ni Allah mshukuriwa, maujudi Mungu wangu
Nashukuru kupokewa, kupokewa dua langu,
Sasa mke nimeoa, naanza maisha yangu
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

8. Leo kwa fadhila zake, zake Rabi msifika
Amenipatia mke, wa sawasawa marika
Neema zimiminike na tujaziwe baraka
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

9. Ndoa ni kitu faradhi, nimeipata nususi,
Nimejipatia hadhi, kwa kuwa na bi arusi
Nimo katika hifadhi, sasa sina wasiwasi
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

10. Mke ampende Mola, afate mambo ya dini
Anitwii bila hila, nikiwa mume wa ndani
Tucheke bila ya dhila, ijapo tumaskini
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

11. Ashike sana ibada, za namna mbalimbali
Atekeze kila muda, kwa zakaa na kuswali
Hayo yanayo faida, malipoye si akali
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

12. Dini ni mali ya roho, mahala pake moyoni
Mwilini ni kama joho, asivuwe asilani
Dini huacha uroho, wa anasa duniani
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

13. Asha apewe subira, asiwe mwenye tamaa.
Aridhike na ngawira, tutakayo ipokea
Tutapokosa sarara, ndondo litasaidia
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

14. Na miye asishindane, kwa kauli za usemi
Wala tusijibizane, ya ovyo kutakalami
Utufanye tupendane, daima yeye na mimi
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

15. Afiche aibu yetu, kama ikitokezea
Asiwe kama upatu, mdomo kucheketukia
Awe mke hasanatu, dini imemkolea
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

16. Ya ndani asiyatoe, hata kama si mazito
Tuyamalize wenyewe, kwa kuzimisha fukuto,
Ndugu zanguni mjue, mto huanza kijito
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

17. Mke ni nguo nyeupe, unadhifu watakiwa
Wa nafsi na makope, yafaa kuangaliwa
Tujitahidi tuepe, kujipakaza madowa

Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

18. Ajiepushe na kutu, iharibuyo nafsi
Inayobomoa utu, tukalingana na fisi
Akitende kila kitu, Unachotaka Qudusi
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

19. Ya Allah Usikatae, kutupa zako neema
Asha nami tupatie, kizazi kilicho chema
Watoto utujalie, waume akinamama
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

20. Tamati sio mtunzi, furaha imenituma
Salamu kwenu wajuzi, kungwi, Mpogo, na thumma
Wamamba, Ame wapenzi, na wengineo ulama
Ndoa ni kitu aula, mwenzenu nimezawiji.

Twaha Ali Nyange, Dar es salaam

Ni kweli ukikosa mke mwema unapata hasara. Kama anavyoimba Sheikh Kaluta Amri Abedi:

1. Rabbi mpe mke mwema, mke mithili ya hurri
Mwenye cheko na huruma, mwenye jamali kathiri
Mwenye kukucha Karima, mchana na asfari
Rabbi Mpatie Hurri, maisha yawe kamili.

2. Mke mbaya ni adha, ya kuungua na nari
Huli ukaona ladha, hulali kwa kufikiri
Japo ulimbue fedha, haikunjuki suduri
Rabbi Mpatie Hurri, maisha yawe kamili.

Mungu bariki, Mwl Twaha Nyange alikamilisha dini yake kwa kumuoa Bi Asha binti Salum Nakuchima. mwalimu Khamisi Sultani Wamwera aliwapongeza wote wawili na kuwakumbusha:

MEZAWIJIANA VYEMA-
MPENDANE KWA TWABIYA

1. Hongera ibini Ali, Twaha Nyange muadhamu
Kuowa jambo halali, ameagiza Karimu
Na Mtumewe Rasuli, katilia umuhimu
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya.

2. Ametamka kuowa, mwongoni mwa sunna zake
Na yule asiyeowa, amekana siyo wake
Hivyo umetenda sawa, uvae usitirike
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya.

3. Ninayo ya kuwambia, machache katika hili
Asakheri yakafaa, kwa kwenu nyote wawili
Ni bora mkipokea, si zigo lilo thakili
Mezawajiana vyema, mpendane kwa twabiya.

4. Sasa umepata mke, nasi umetujulisha
Kwa mapenzi umshike, na njia kumuonesha
Wewe ni mwalimu wake, juu yako kufundisha
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

5. Kuoa na kuolewa, ndiyo moyo wa salama
Ketini mle uluwa, huku mwamcha Rahima
Ninyi mmejichopoa, kwenye lindi la nakama
Mmezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

6 Msiwe mbali na dini, dini ndiyo muhimili
Mbele itangulizeni, na mshike maadili
Msiache abadani, Islam ni asili
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

7 Ishini vyema nyumbani, msiiache ibada
Allah mtegemeeni, vinyamkela si ada
Mwombeni Mungu watini, lieni kwenye sujuda
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

8 Mpeni roho Manani, kwa dini kipaumbele
Akiwajia shetwani, kuwambia lele lele
Haraka mfukuzeni, kwenu asifanye shule
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

9 Mola Atakayo kwenu, ukhalisi wa imani
Yalo masurufu yenu, matendo mema fanyeni
Hiyo ikawa sakunu, mkaingizwa peponi
Mmezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

10 Allah Atakacho kwenu, mtowe babu amana
Kutoka mapato yenu, kiasi cha kulingana
Na yeye Muumba wenu, Atawajazia tena
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

11 Mkipata matulubu, ya halali na manono
Muwe na nyoyo twayibu, mtowe kwa wingi mno
Mrejeshe kwa Wahabu, hizo fedha na mavuno
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

12 Narudia ndugu zangu, tunzeni vyema baitu
Washufuni walimwengu, wale waitwao watu
Hupenda sana vurugu, ijiri kwa kila mtu
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

13 Kaeni kwa utulivu, msigombane gombane
Kuweni wavumilivu, sana mvumiliane
Kamwe msiwe watovu, kwa khuluka mlingane
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

14 Mdhibiti sana ndimi, zungumzeni ya raha
Ambizaneni kwa semi, laini na kwa furaha
Mkosapo mjihami, muombane msamaha
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

15 Kauli mbaya hasara, huko msifikishane
Inawakisha hasira, mikononi mtiane
Bali hekima busara, hujenga mara nyingine
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

16 Msiwe wa kukindana, wa mambo haipendezi
Bora kushauriana, wawili ninyi azizi
Mwisho taafikiana, kwa huba na kwa mapenzi
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

17 Msitumie lafidhi, inayokata maini
Mwenzio ukamuudhi, ndowa akailaani
Mpe heshima na hadhi, mafunzo ya Qur'ani
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

18 Jiepusheni ghadhabu, hasira na munkari
Kwa mbali mjitanibu, vitaondowa uzuri
Mjifanye kama bubu, hali waneni mahiri
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

19 Wewe na wako mwandani, kila mmoja ni tunu
Mungu Awafadhilini, Abariki ndowa yenu
Awape wana makini, wa kuendeleza vyenu
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

20 Kwa leo haya yatosha, hadhari msiiache
Kwa hiyo ninafupisha, siri yenu muifiche
Kwake Asha dhihirisha, na yake asikufiche
Mezawijiana vyema, mpendane kwa twabiya

Al-Ustadh Hamisi S. S. Wamwera
Mbagala Kimbangulile - Dar es salaam

Naye kiumbe mzito, Pazi mazongera alishangilia:

SHUMBE TWAHA

1 Hongera Twaha wa Nyange, kuoa jambo la kheri
Ulipate lako tonge, kutoka kwake Kahari
Akuepushe sarange, ndoa iwe makuburi
Haya Mapenzi ya Mungu, baraka twakuombea

2 Wakimbie vitatange, waone kama shubiri
Wajipambe kwa vitenge, siyo yetu desturi
Wavae ngozi za kenge, Rabi muepushe shari
Haya Mapenzi ya Mungu, baraka twakuombea

Pazi Mazongera (Kiumbe mzito), Dar es Salaam

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MANDHARI YA MWISHO

Akainua mikono yake kwa maombi ya kimya, na wote waliokuwapo msikitini nao wakafanya hivyo. Kila mmoja akajawa na maono na mara moja msikiti ukawa nyumba ya vilio. Maombi yakaendelea kwa muda na yalipomalizika nyoyo zikawa zimetulia. Sahibzada Sahib akasisitiza kwamba awezaye afunge saumu kesho. Kisha akaondoka kwenda nyumbani kwa Nawab Muhammad Ali Khan r.a. Lakini hakuwa na utulivu na akapenda kuomba dua katika upweke. Akaenda huku akimwomba Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a. awe macho ili mtu yeyote asimfuate kwani ataka kuwa katika upweke. Alikuwa akipita bustanini haraka haraka ambapo Maulawii Muhammad Ali akapata kumwona kutoka mbali na kumjia upesi pamwe na marafiki zake na kumshughulisha katika maongezi. Wakaendelea kutembea juu chini wakiongea kwa bidii hadi adhana ya sala ya magharibi ikatolewa.

Baadaye Sahibzada Sahib r.a. akaeleza kwa kifupi maongezi hayo kama ifuatavyo:

Maulawii Muhammad Ali:

"Mambo yote huamuliwa vizuri katika kushauriana. Baada ya Hadhrat Khalifatul Masih r.a. kwisha kufariki lolote lisiamuliwe kwa haraka. Kupatikane kushauriana kikamilifu."

Sahibzada Sahib r.a.:

"Haraka haifai, na hakuna budi kushauriana. Watu wengi wanaendelea kuwasili na mpaka kesho idadi kubwa itakuwa imefika. Wanajumuiya waongozi wanaishi karibu sana, watawasili hadi kesho. Kushauriana kwawezekana baada ya hao kufika."

Maulawii Muhammad Ali:

"Haraka hiyo haipendezi. Kwa kuwa zipo hitilafu, uamuzi ufanywe kwa umoja baada ya kujadiliana kikamilifu. Yafaa Jumuiya nzima ifikirie jambo hili kwa miezi minne au mitano. Kisha kupatikane kubadilishana maoni ndipo uamuzi wowote utakaofanywa utekelezwe."

Sahibzada Sahib r.a.:

"Swali la kwanza ni: Kuna hitilafu zipi? Swali la pili ni: Kama katika muda huo kutokee uchafuzi katika Jumuiya, nani atakuwa mwenye madaraka pasipokuwa Kiongozi? Watu waliojumuika alipofariki Masihi Aliyealhidiwa a.s. walishauriana mara moja na kuamua. Njia hii ilifuatwa hata katika nyakati zilizopita. Kulikuwa hamna muda wa miezi sita kungoja kabla ya ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. au baadaye."

Maulawii Muhammad Ali:

"Zamani hitilafu hazikuwepo, sasa hitilafu zipo. Tena, kuna shida gani katika kungoja kwa muda fulani? Kuna nini *Khalifa* anayolazimika kufanya kesho?"

Sahibzada Sahib:

"Alipofariki Masihi Aliyeahidiwa a.s., Jumuiya iliamua kwamba *Ukhalifa* uwepo katika Jumuiya. Haina haja ya kushauriana juu ya swala hili tena, wala haliwezi kuletwa sasa. Kushauriana kwaweza tu kuhusu nani apaswa kuwa *Khalifa*? Ama swali lako kwamba: Ni nini anayolazimika *Khalifa* kufanya kesho? Jibu lake ni kwamba zaidi ya kuangalia hali ya kiroho, ni kazi ya *Khalifa*, kuweka Jumuiya katika hali ya umoja na kuilinda dhidi ya machafuko, na utekelezaji wa kazi hiyo si kitu cha kuonekana ili nikutolee mifano. *Khalifa* hana budi kuipatia Jumuiya malezi ya kiroho na kudumisha nidhamu. Malezi ya kiroho si kitendo cha kiwiliwili kinachoweza kuonyeshwa, wala machafuko hayana wakati maalum hata isemwe hayawezi kutokea kabla ya tarehe fulani. Yawezekana kesho litokee jambo fulani linalohitaji mwenye kuongoza. Hivyo, achilia mbali swali hili kwamba *Khalifa* awepo ama hapana. Kushauriana kwaweza kufanyika kwamba nani atakuwa *Khalifa*."

Maulawii Muhammad Ali:

"Sasa hili lazusha tatizo. Kwa sababu kuna hitilfafu katika itikadi, basi kutakuwa hitilafu katika uchaguzi wa mtu. Hatuwezi kufanya baiati ya mtu tunayehitilafiana naye katika itikadi."

Sahibzada Sahib r.a.:

"Nielewavyo mimi, hitilafu haiendi mbali sana mpaka iwe kizuizi kufanya baiati ya mtu wa upande mmoja au wa pili. Kwa vyoyote tuko tayari kufanya baiati ya mmojawapo miongoni mwa kundi lako."

Maulawii Muhammad Ali:

"Hii ni ngumu. Wapaswa kutafakari zaidi na kushauriana nyinyi kwa nyinyi, na kesho tukutane tena."

Kwa kufuata pendekezo hilo la Maulawii Muhammad Ali, Sahibzada Sahib akaorodhesha majina sitini na akamwomba Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a. awaite hao ndugu ili kuhudhuria katika mkutano usiku huo kwa kushauriana. Baada ya kushauriana, wote wakakubali kwamba kabla hajazikwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., *Khalifa* mwenye madaraka kamili



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

achaguliwe ambaye atapanga mazishi. Pia ikakubaliwa ya kwamba usiku huo maombi yafanywe ili Mungu kwa fadhili Zake Aridhie kuidumisha Jumuiya katika njia iliyonyoka na kuijaalia kukanyaga njia za radhi Yake, na kwamba kesho wote wafunge saumu na maombi maalumu yaendelee.

Keshoye, saa za adhuhuri Wanajumuiya zaidi ya elfu moja walikuwa wamewasili Qadian kutoka nje. Sahibzada Sahib r.a. akashauriana na watu wa familia yake kuhusu hali iliyozuka. Baadhi yao walikuwa na maoni ya kuendelea kueneza itikazi walizoamini kuwa sawa, na kwa shabaha hii wakahisi kwamba hakuna budi *Khalifa* kuwa yule anayeafikiana nao katika itikadi hizo. Lakini Sahibzada Sahib akasisitiza kwamba kuhifadhi umoja wa Jumuiya ni muhimu kabisa. Katika rai yake, uchaguzi wa *Khalifa* ni wajibu wa kidini. Kama hii ikubaliwe, basi njia ifaayo sana ni kumchagua *Khalifa* kwa kupigwa kura na wale waliopo. Kama hiyo haikubaliki, wote waafikiane kumteua mtu baki. Kama hiyo nayo ikishindikana baiati yaweza kufanywa kwa yule anayekubaliwa na kundi la pili au mmojawapo miongoni mwao. Hatimaye watu wote wa familia yake wakakubaliana na pendekezo lake.

Hapo ndipo ujumbe ukapokelewa kutoka kwa Maulawii Muhammad Ali ya kwamba anataka kuendelea na maongezi ya jana. Akaombwa afike hapo. Akawasili pamwe na baadhi ya marafiki zake. Wakati huo, Sahibzda Sahib r.a. alikuwa na Maulawii Muhammad Ahsan r.a., Nawab Muhammad Ali Khan r.a. na Dkt. Khalifa Rashiduddin r.a. pamoja naye. Maongezi yakashika njia ili ile ya jana. Yakazuka pia mabishano kuhusu hitilafu za itikadi baina ya Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan r.a. na Maulawii Muhammad Ali, lakini Sahibzada Sahib r.a. akayakomesha, na akamwuliza Maulawii Muhammad Ali itakuwaje ikiwa mwafaka unashindikana baada ya kupita kipindi kirefu asemacho? Kama hapo uamuzi utafanywa na watu wengi, kwa nini watu wengi hawawezi kuamua sasa?

Huko nyuma watu wakajumuika katika Masjid Nur, nao walikuwa na mahangaiko. Ikaonekana kwamba baada ya Machi 4, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alipoandika wasia na akafanya usomwe na Maulawii Muhammad Ali mara tatu, ambamo alikuwa ameandika kwamba *Khalifa* ajaye hana budi kuwa na sifa fulani ndani yake, Maulawii Muhammad Ali akatayarisha kijitabu ambamo haja ya *Khalifa*, inavyofahamika kikawaida, ikapuuziliwa mbali. Kijitabu hicho kilipigwa chapa na nakala zake zikatumwa kwa marafiki zake pamoja na maagizo ya kuzizagaza mara habari ya kifo cha Hadhrat Khalifatul Masihi ikipokelewa. Kila mmoja aliyewasili Qadian baada ya kupata habari yenye kuhuzunisha sana ya kufariki kwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa amepatiwa nakala yake safarini. Watu wengi sana wakakasirikia propaganda hiyo mbovu na ya ovyo. Na kila mmoja akapenda uchaguzi wa *Khalifa* ufanywe haraka.

Mazungumzo yalikuwa hayasongi mbele, na mlango ukabishwa mfululizo kwamba zengwe limalizwe haraka. Sahibzada Sahib r.a. akapendekeza ya kwamba kwa kuwa hakuna matumaini ya kupatana, hivyo yapaswa wote waondoke waende Masjid Nur na mashauri yafanywe na wale waliokwisha jumuika tayari huko. Hapo Maulawii Muhammad Ali akafoka: "Wasema haya, kwani wajua watamchagua nani."

Sahibzada Sahib r.a.: "Kinyume chake, niko tayari kufanya baiati ya yeyote miongoni mwenu."

Maulawii Muhammad Ali: "Hata hivyo unaelewa wafikirivyo."

Sahibzada Sahib r.a. sasa akawa na yakini kabisa kwamba mwafaka hauwezekani. Basi akasema: "Twaamini kwamba ni wajibu wa kidini kudumisha *Ukhalifa*, lakini unafikiri *Khalifa* hahitajiki. Hitilafu hii haiwezi kupatanishwa. Uko huru kufanya upendavyo. Sisi tutashauriana na kufanya baiati kwa yule tunayeafikiana juu yake.

Kikao kilimalizika kwa maneno hayo. Sahibzada Sahib na wenzake wakaelekea Masjid Nur ambako mkusanyiko wa watu kati ya elfu moja mia tano na elfu mbili walikuwa wanawasubiri. Sahibzada Sahib akawasalisha sala ya alasiri, kisha Nawab Muhammad Ali Khan r.a. akawasomea wasia wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. wa Machi 4, 1914, aliomkabidhi yeye na akaongeza: "Nimekwisha toa amana ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. Sasa ni juu yenu kutenda sawa nayo." Tangazo lake likapokelewa kwa kelele za "Hadhrat Mian Sahib, Hadhrat Mian Sahib" kutoka kila upande. Katikati ya kelele hizo akainuka Maulawii Seyyid Ahsan r.a. na akapaza sauti: "Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema kunihusu mimi kwamba mimi ni malaika mmojawapo kati ya malaika wawili waliotajwa katika Hadithi kwamba Masihi atateremka katika zama za mwisho akiegemea juu yao. Mimi nafikiri Sahibzada Bashiruddin Mahmud Ahmad anastahili kabisa kwa kila jiha kuchukua baiati yetu, nami namwomba atupokelee baiati yetu. Hapo Maulawii Muhammad Ali na Seyyid Hamid Shah r.a., wote wawili, wakainuka, ikaonekana wanataka kusema kitu, na wakaanza kuzozana nani aseme kwanza. Waliopo hawakuwa na moyo wa kuwafurahia, na Sheikh Yakub Ali Irfani r.a. akaeleza maono ya watu wote kwa kusema: "Wakati ni wenye thamani sana wala hauwezi kupotezwa kwa mizozo ya aina hii. Mpenzi wetu, tafadhali kubali baiati yetu." Hayo yalipokelewa kwa kelele za *Labeka, Labeka,* na watu wakaanza kusonga mbele upande wa Sahibzada Sahib. Hapo wale wachache wenye shauri jingine wakaondoka. Hakuna aliyewazuia.

Kimya kikaushika mkutano, ingawaje kila mmoja alikuwa na kiherehere cha kumsogelea karibu zaidi Sahibzada Sahib r.a. Yeye akakaa kimya kana kwamba anashughulikia maombi. Qadhi Amir Husain, Sheikh mheshimiwa, akamwendea akihangaika sana na kamwomba: "Hudhur, tafadhali kubali baiati yangu." Sahibzada Sahib akaangalia juu, macho yake yakimtafuta mtu fulani. Akamgundua Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a. aliyekuwa amebanwa baina ya msongamano wa watu wenye shauku na kumwambia: "Maulawii Sahib, jukumu hili zito nimebebeshwa ghafla isivyotazamiwa. Sikumbuki masharti ya baiati. Tafadhali nieleze hayo." Basi kuchukua baiati kukaanza. Hadhrat Khalifatul Masihi II akatamka maneno ya baiati kama yalivyonenwa na Maulawii Seyyid Mohammad Sarwar Shah r.a., na kila mmoja akarudia hayo kufanya baiati. Maneno ya baiati ndiyo haya:

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Mapango ya As-habul Kahf

Na Mwalimu Abdullah Khamisi Mbanga – Dar es salaam

Kutoka toleo lililopita

Mapango haya yapo karibu sana na Khirbet Qumran monastery nyumba ya watawa idhaniwayo kuwa ilikuwa ndiyo makao ya Waesini (Essenes) na miswada mingi iliyopatikana humo ilikuwa na maelezo ya Kikristo, ingawa ilipuuzwa. Inafikiriwa kwamba miswada hiyo ililetwa katika mapango haya wakati viongozi wa kidini walipokuwa wanahama kutoka jengo la Khirbet Qumran kukimbia wanajeshi wa Kirumi mnamo mwaka 70AD, lakini haifahamiki kama mapango hayo yalikuwa yakitumika kabla ya hapo.

MAPANGO YA MISRI

Kuna maandiko ya kidini ya Nag Hammadi ambayo yaligunduliwa mwishoni mwa vita vikuu vya pili karibu na mto Nile, yalimilikiwa na kikundi cha Wakristo tangu karne ya 4. Maandiko haya yalikutwa katika mtungi uliolakiriwa ukiwa chini ya udongo. Ukiwa umehifadhiwa kwa namna ile ile ya Red sea scrolls kule Qumran. Misahafu hii ilifichwa humo katika zama zile za mateso ya Wakristo dhidi ya Wakristo wenzao. Bila shaka Kanisa katika Misri liligawanyika makundi mawili makubwa katika wakati ule, Orthodox na monophysite, makundi haya yalitofautiana kuhusu suala la utatu mtakatifu.

Kuna ushahidi mwingi wa kihistoria juu ya mateso dhidi ya Wakristo katika Misri. Waliteswa chini ya Mfalme Severus (222-235AD), ambapo Wakristo walikamatwa, kuhojiwa, kuteswa na kuuawa huko Alexandria. Wakristo wa Monophysite walikuwa wakipinga utatu, hivyo Ukristo wao ulikuwa mbali sana na ule wa Ulaya na kwa hivi hawa wakawa ndio waathirika wakuu wa mateso ya zama hizo.

Inasisimua mno kuona kuwa karibu na mahala ilipogunduliwa ile misahafu ya Nag Hammadi kumekutikana msururu wa makaburi kutoka katika kizazi cha sita cha ufalme wa Pepi I na II ambao walitawala mwaka 2350 – 2200 BC.

Makaburi hayo ya mawe, yalifukuliwa yakabaki yakabaki matupu na kutumiwa na viongozi wa Kikristo kama maficho yao wakati huo wa mateso, inawezekana Wakristo hawa ndio walioficha misahafu hiyo iliyogunduliwa ya Nag Hammadi. Pia ndani ya mapango hayo kuligunduliwa michoro ya msalaba na tafsiri ya



Mwl. Abdallah Mbanga

Zaburi kwa lugha ya Kikopti.

Hao wa Monophysite inasemekana walianza kuteswa kwa ajili ya imani yao kunako karne ya 7, na hivyo kutokana na imani yao kuwa ya umoja wa Mungu iliwawia rahisi mno kuupokea ujumbe wa Islam kuliko Ukatoliki wa Roma. Mapango hayo yako pembezoni mwa miinuko iliyo karibu na mto Nile, na kwamba mbele kidogo ya eneo hilo kuna eneo la Oxyrhynchus ambako yaligunduliwa maandiko meingine ya Kibiblia.

HITIMISHO

Kama inavyoonekana, kuna mkanganyiko mkubwa baina ya wanahistoria wa Kiyahudi na Kikristo kuhusiana na matumizi ya mapango na kuhusu wakazi wa mapango. Aghalabu pale ilipotokea tofauti ya maoni baina yao waliamua kuwaita watu wa pango kuwa ni Wayahudi Wakristo, ambao walichukua sura mbalimbali kama vile, Waebioni na Wanazarayo, na wale ambao walishikilia imani ya umoja wa Mungu. Watu hawa walikuwa ndio walengwa wakuu wa mateso kutoka sehemu tatu, Warumi, Wakristo wa Orthodox na Wayahudi. Makundi hayo yaliwahesabu hawa kuwa ni watu waliopotosha uelewa wa dini yao.

Inawezekana kabisa kwamba ugunduzi mwingine zaidi unaweza kutokea kama ulivyotokea ule wa Nag Hammadi na Qumran ambao bila shaka ni wa hivi karibuni tu (1945) millennia mbili baada ya kufichwa kwake. Na kwa yakini taarifa zaidi bado zinahitajika kuhusu mapango ya Emesa huko Syria, ambako ni karibu mno na Antiokia mahala panapodaiwa kuwa imani ya umoja wa nguvu ilikuwa na mashiko makubwa.

Na ama kuhusu matumizi ya mapango kama sehemu za maficho kwa watu waliosigana imani na jamii si jambo geni kihistoria. Inaonekana kuwa mapango yalikuwa makimbilio maarufu kwa watu ambao waliazimia kujitenga na harakati za uma wa zama zao. Ndio maana hata zama za Mtume (saw) pango la Hira (Jabal Hira) lililo maili kadhaa kutoka Makka lilitumika kama sehemu ya kujitenga ya Mtume (saw) baada ya kutokubaliana na mwenendo wa jamii iliyomzunguka. Hali kadhalika katika nyakati za mwanzo za Islam Waislam waliwahi kuishi eneo la bonde lililojitenga liitwalo Shabi Abu Talib baada ya kususiwa na watu wa Makka.

Bila shaka yoyote uchunguzi pia unahitajika kuhusu mapango yetu kama yale ya Amboni, Matombo na mengineyo ambayo huenda yalitumika na watu wa kale kama sehemu zao za miji zilizojitenga na jamii ya zama zao. Katika mapango hayo kuna viashiria vingi vya maisha ya kale, kama vile michoro, sanamu, samani n.k

Haya yote yanaonyesha kuwa kudhani kwamba As-Habul Kahf walikuwa wafu katika mapango ni dhana isiyoingia akilini na isiyo na ushahidi wowote wa kihistoria na juu ya hayo inapingana na mafundisho ya Qur'an Tukufu ya kwamba wafu hawarudi duniani (39:43).

Sheikh Kaluta Amri Abedi na Jiji la Cairo

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam

Kutoka Toleo lililopita

Si kila mara ukwasi, huleta raha kamili
Pia huleta nuhusi, kusababisha ajali
Na kupigwa muflisi, wakakuambaa mbali
Walokupenda awali, zama zile za maraha

Au hujakuta watu, walokiambwa rijali
Waliohizini vitu, kwa wingi bila mithili
Sasa waitwa vijitu, na kuonwa baradhuli
Hungedhania asili, walipata onja raha

Mengi tuitayo raha, ni mauzauza bali
Ni fupi zake furaha, zingawa na bei ghali
Raha ya kweli kifaha, ni kumtii Jalali
Na kuambaa batili, ndipo uipate raha.

Lahaula! Maneno yenye waadhi na hekima yakaeleweka vibaya. Bahari ya ushairi ikachafuka. Dhana mbovu na chafu zikatawala. Wa mstari wa mbele waliong'aka kuhusu shairi hilo ni washairi wa Dodoma. Khamisi Amani Khamisi (Nyamaume) na Mahmood Hamduni (Jitukali). Nyamaume alilaumu;

Kalamu tungali nazo, usambe zimekatika
Tuyaonapo mauzo, kujibu hatuna shaka
Mafumbo na mageuzo, si yenye kutuzunguka
Mtego uliomshika, kesho utashikwa wewe

Naye Jikali akaingia kati na kuimba;
Nakujua una huba, nadhani ni badiliko
Badiliko la kushiba, kwa dalili ya tamko
Njia yetu ina miba, mwakichafua kivuko
Dunia ni mzunguko, jua dunia duara

Sheikh Kaluta Amri Abedi alipata watetezi. Mshairi wa Dodoma Mathias Mnyampala (Pendachako) hakukubaliana nao. Yeye aliwakumbusha kwamba Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa mcha Mungu ambaye hawezi kudiriki kushangilia yaliyomsibu mtu. Yeye alikumbusha nini hasa ni kazi ya shairi;

Huwadibu walimwengu, ili wawe na hadhari
Yawaepuke machungu, masahibu na jibari
Na kumpendeza Mungu, kuvuta njema sururi
Ni waadhi ushairi, wenye nemsi na machungu

Kijana wa Tanga Mohamedi Alli Al-Bukhri anayetokana na ukoo wa washairi maarufu nchini aliwakumbusha;

Kwa ghafula mnang'aka, na mengi mno mafoko
Na masombo kujivika, majasho mtiririko
Silioni lililozuka, la kuwatia sumbuko
Dunia ni mzunguko, mtego umefatuka

Naye Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa maneno ya hekima aliwakumbusha washairi wenzake hatari za dhana, naye akaimba;

Dhana jambo la hatari, hasa kwa mtu ghaidhi
Neno na liwe la heri, hulipindika kukidhi
Muradi wa kuaziri, na kujikuzia hadhi
Kwa mwingi utaaradhi, wa usaliti na shari

Hasa akiwa jahili, huzidi haya maradhi
Kila usemi sahili, kwake ni fimbo ghamidhi
Huzuka kuliwali, na kujinaki ukadhi
Wa kujua alfadhi, ambazo za mizingili

Basi tazama kivumbi, atakapo kuaridhi
Hutiana kila fimbi, ukapotoa lafidhi
Na mimacho tumbitumbi, ya kijicho na maudhi
Uzushi yake faradhi, fitina wake ukumbi

Wanazuoni shairi, hizi wako nazo radhi
Ni tungo za umahiri, tutoleazo waadhi
Si zumo lilodhihiri, kuwa lengo la gharadhi
Mambo haya tunahodhi, katika kila dahari

Twajikinga kwa kahari, Mbora wa kuhifadhi
Na kila dua ya shari, ya wenye nyoyo ghalidhi
Na shuku za kiayari, za wenye kilima fadhi
Na fitina mfawidhi, za komba wa kila pori

Ni bahati mbaya sana shairi hili lilieleweka vibaya, labda ni kutokana na mazingira halisi yaliyojitokeza wakati huo. Bwana mmoja maarufu Chifu Abdallah Saidi Fundikila alikuwa amepatikana na kashfa ya kupokea mlungula. Chifu Fundikira aliheshimika sana nchini na alikuwa kiongozi wa kabila la Wanyamwezi. Ilikuwa patashika Tabora na Dar es salaam. Wanyanyembe kwa mamia walifurika Dar es salaam kuja kusikiliza kesi ya Mtemi wao. Ajabu kuliko zote watu waliomtuhumu Sheikh Amri Abedi; "Kufurahia msiba wa mwenzio" ndiye aliyetoa ushahidi mzito wa utetezi kwani alisema koritini ya kwamba huyo Mhindi aliyesema amempatia mlungula Chifu Abdallah Saidi Fundikira hakuwa amesema kweli, kwani siku hiyo aliondoka naye katika ndege wakielekea Tabora. Ni ushahidi huo uliomuokoa Chifu Abdallah Saidi Fundikira na kubadili mwelekeo wa kesi hiyo. Hadi ikagunduliwa ya kwamba hizo zilikuwa ni njama tu za kisiasa.

Umajumui (Pani Africanism) wa kiafrika ni ukuaji wa umoja na maelewano miongoni mwa watu weusi; kujitambua kwamba Mwafrika amedharauliwa. Mshikamano huu umewajumuisha watu wote wenye asili ya Afrika na wale wanaojihesabu ya kwamba Afrika ni kwao. Madhumuni ya umoja huu ikawa kurejesha heshima ya mwana wa Afrika, kupigania uhuru wa bara la Afrika na kuleta muungano wa bara la Afrika. Hiyo ndiyo iliyokuwa sera ya chama cha TANU na Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa ni mwanachama maarufu wa chama hicho hadi kufikia hatua ya kuwa mjumbe wa halmashauri kuu ya chama hicho. Kutokana na imani yake ya ukombozi na muungano wa Afrika, mwaka 1956 chama cha TANU kilipeleka ujumbe katika mkutano wa nchi huru za kiafrika za wakati huo na vyama vya siasa vilivyokuwa vinapigania ukombozi wa bara la Afrika. Ujumbe wa TANU uliongozwa na Bw. Oscar Kambona Katibu Mkuu, wakiwemo Rashidi Mfaume Kawawa, Nsilo Swai, na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Ujumbe wa TANU ulichangamsha katika kikao hicho kilichofanyika Tunisia. Kwa sababu mjumbe wa TANU aliweza kuhutubia katika lugha ya Kiarabu akieleza umuhimu wa umoja wa Afrika na aliwaeleza pia ya kwamba wakati ulikuwa umefika wa kutumia lugha zao za asili na zikaelezwa juhudi za Watanganyika katika kukuza na kuendeleza Kiswahili.

Mwaka 1960 unakumbukwa kuwa ni mwaka wa uhuru wa Afrika. Nchi nyingi zilipata uhuru. Hapo wazo la muungano wa nchi huru za Kiafrika likashika kasi. Mwaka 1963 ukaanzishwa umoja wa nchi za Kiafrika katika jiji kuu la Ethiopia Adisababa. Ilikubaliwa ya kwamba viongozi wa Afrika wawe wanakutana kila mwaka mara moja na mkutano uzunguke kutoka nchi moja hadi nyingine. Ilikubaliwa mwaka 1964 mkutano wa kwanza wa nchi huru za Kiafrika ufanyike mjini Cairo. Nchi ya mwanamapinduzi Ghamal Abdul Nasser ambaye alikuwa ametoa mchango mkubwa kwa ukombozi wa Afrika. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na mshauri wake mkuu katika mkutano huo alikuwa ni Sheikh Kaluta Amri Abedi. Ulikuwa ni mkutano uliowakutanisha miamba wawili wa Afrika Julius K. Nyerere na Kwame Nkurumah walipopambana kwa kutumia hoja.

Viongozi wote hawa wawili waliwahi kuwa waalimu na kupata elimu ya juu. Nyerere akiwa amesomea Edinburg -Scotland na Kwame Nkurumah akiwa amesomea chuo kikuu cha Lincoln Marekani na London School of Economics Uingereza. Wote walikuwa wanaendesha vyama vilivyokuwa vinapendwa na wanachi. Nkurumah CPP na Nyerere TANU. Wote walikuwa mahiri katika kutumia kalamu na mabingwa wa utoaji hotuba. Safari hii Kwame Nkurumah alijifunga kibwebwe kummaliza Nyerere. Ubishi mkubwa ulizuka ambao ungemalizwa kwa maneno laini na maelewano. Lakini haikuwa hivyo Tanzania ilishambuliwa kuwa ni kichaka cha ukoloni mamboleo. Mahali ambapo njama zinafanywa ili kucheleweshe ukombozi wa Afrika. Maneno hayo yalimuudhi na kumchefua kijana wa Kizanaki Nyerere. Alisikitika kiasi hiki ya kwamba akauomba ujumbe wa Tanzania ukapumzike kwanza katika hoteli walipofikia. Nyerere alionekana bado amekasirika na akamuomba Sheikh Kaluta Amri Abedi atayarishe jibu. Nyerere alifahamiana fika na Sheikh Amri, alimaizi uwezo wake wa kujenga hoja, alikumbuka alivyokuwa anambwaga kihoja kule shuleni kuhusu masuala ya dini. Alikumbuka jinsi Waahmadiya wasivyo na hasira wakati wa kujibu hoja. Alikumbuka Sheikh Amri alivyojenga hoja na kuwashinda wale wabunge katika bunge la Tanganyika ambao walikuwa wanasisitiza ya kwamba watu weupe wafunge virago vyao na kuondoka nchini. Naye akawa ametoa tishio kwamba angeweza kujiuzulu iwapo muswada huo ungeweza kupita. Alikumbuka pia utenzi wa Sheikh Amri uliosema;

"Wao Waasia pia wazungu,
Wote ni raia katupa Mungu
Tutawaangalia wasile chungu,
Tuwape kafungu ka utawala

Akakumbuka alivyomuacha hoi Sheikh Saleh Abdallah Farsy katika ***'Uongofu wa tafsiri wa Qur'an Tukufu na husuda ya Sheikh Saleh Abdallah Farsy'***.

Endelea uk. 9

Nuru ya Fasihi imezimika Afrika

Na Mahmood Hamsin Mubiru
- Dar es Salaam

Nuru ya Fasihi iliyowaka barani Afrika imezimika. Ni giza totoro. Mzungupule aliyetuonesha wapi mvua ilipoanza kutunyeshea hatunae. Sijui tutakauka lini? Wapi tutapata maneno yenye uwezo na ithibati ya kuchimba katika nafsi zetu na hatimaye kudhihirisha maumivu tuliyoyapata kutokana na kuondokewa na kito hiki cha thamani. Mkongwe katika Riwaya. Mtunzi wa hadithi fupi na Mshairi mahiri Chinua Lumogu Achebe aliyefia mbali kabisa na bara alilolipenda Afrika.

Mapambano ya kulikomboa bara la Afrika yalichukua sura mbili. Walikuwapo wale waliotafuta Ufalme wa kisiasa, kupandisha bendera na kupigiwa mizinga ishirini na moja. Hao ni akina Sekuture, Ben Bela, Kwame Nkurumah, Julius Nyerere kwa kuwataja wachache. Kwa upande wa pili ambao labda ni mbaya kuliko ule wa kuteka nchi, ni ule wa kuteka akili zetu na fikra zetu. Kusafisha kabisa bongo zetu na kuamini sisi si watu na wala hatukuwa na historia wala utamaduni. Ukombozi huu wa pili uliongozwa na waanzilishi wa Negritude pamoja na Umajumui (Pan Africanism),ambayo



Chinua Achebe 1930 - 2013
baba wa Fasihi Afrika

ilianzishwa na ndugu zetu wa Amerika wenye asili ya Afrika.

Kwa Afrika iliyotawaliwa na Muingereza aliyepeperusha bendera ya kujenga utu, na heshima ya Muafrika si mwingine isipokuwa Chinua Achebe. Ni vigumu sana kusahau Riwaya yake iitwayo *Things Fall Apart* na kutafsiriwa katika Kiswahili kuwa '*Hamkani si Shwari tena*'. Riwaya hii ni hoja madhubuti inayosherehekea utu wa mtu mweusi, utamaduni wake na heshima yake. Ni kwa kiasi gani alifanikiwa kuwaibisha waandishi kama Joseph Conrad katika '*Heart of darkness*' na Graham Green walioamini ya kwamba Afrika ilikuwa bara la giza kabla ya kuja kwa Wazungu.

Ni Chinua Achebe aliyehakikisha ya kwamba hayo yalikuwa ni masingizio yasiyo miguu wala kichwa. Na ni yeye aliyerudisha heshima ya mtu mweusi kwa kutumia kalamu.

AMETAWAFU ACHEBE

1 Hae msiba mzito, ametawafu Chinua
Aliyelea watoto, waloacha yetu ndia
Warudi kwenye fukuto, la mizizi asilia
Vipi utakuwa mtu, ukiibeza asili?

2 Kwa kutumia kalamu, mengi katuandikia
Yepi tufanye yadumu, katika yetu jamia
Achebe hasa Mwalimu, katufunza kwa hatua
Visome kwa tamakuni vitabu aloandika

3 Mapenzi yamenizidi, kaditamati natoa
Dua tupate idadi, waandishi wenye nia
Wailinde yetu jadi, mwisho isije potea
Achebe wengi lukuki, twawataka Afrika

(Itaendelea toleo lijalo)

Sheikh Kaluta na Jiji la Cairo

Kutoka uk. 8

Ulikuwa ni ushindi wa Tanzania. Sheikh Amri aliitengeneza kweli kweli hotuba hiyo. Akitumia lugha ya istihzai na vijembe hadi akalipasua joho la Nkurumah na nyumba ya hoja aliyokuwa ameijenga Kwame Nkurumah ikawa dhaifu mithili ya 'Ankabuti'. Hotuba ilianza taratibu huku akichomekeza utani kwamba bila ya waganga wa mvua kutoka Afrika Mashariki, Wamisri wasingekuwa na ubavu wa kuwa wakarimu. Nyundo ikaanza kugonga kwamba watu wako tayari kutumia akili zao nyingi walizopewa ili mwanahistoria mjinga afikiri ya kwamba wao peke yao ndio waliokuwa wanataka umoja wa nchi za Afrika kuliko wengine. Alisema hilo haliingii akilini. Wakati Nkurumah akitaka muungano wa nchi za Kiafrika mara moja, Nyerere alisema kwamba haraka haraka haina baraka, lililo zuri ni kwenda taratibu. Nchi jirani ziungane na upatikane uzoefu, zishirikiane katika uchumi. Na msumari wa mwisho na uliofanya kikao chote kiangue kicheko hadi kutokwa na machozi ni pale aliposema 'nchi moja iko tayari kumega kipande cha ardhi cha nchi jirani, kwa kisingizio cha umoja wa Afrika. Hili lilikuwa ni dongo kwa Ghana iliyokuwa inataka kupora sehemu ya Togo.

Nyerere alimaliza hotuba hiyo huku akishangiliwa na viongozi wote wa Afrika na ujumbe wa Tanzania ulikuwa na tabasamu. Kukumbatiana na vicheko. Kalamu ya Sheikh Kaluta Amri Abedi ilikuwa imemuangusha Kwame Nkurumah. Na waliokuwepo mmoja wapo Michael Kamaliza alisema lilikuwa pigo la nguvu na mwanguko wa mende. Mapambano hayo yanabaki kuwa somo kubwa kuwa kinachotakiwa ni ujengaji wa hoja na siyo kupayuka.

Ni bahati mbaya kila palipo na furaha hapakosi huzuni. Ni katika moja ya dhifa walizofanyiwa huko Cairo ndiko Sheikh Kaluta Amri Abedi alipokula chakula ambacho ghafla kilifanya afya yake ibadilike hadi kupelekwa Ujerumani ambako alifariki tarehe 09 Novemba 1964. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

Mwenyezi Mungu Huwapatia waja wake elimu ya ghaibu kuhusu mambo fulani fulani. Kulikuwepo na kidokezo kuhusu kifo cha Sheikh Kaluta Amri Abedi mara baada ya ugonjwa wake. Sheikh Inayatullah Ahmadi ambaye hapo mwanzoni alikuwa askari na baadae akaingia katika kazi ya ubashiri aliona katika njozi ya kwamba wanaongozana na Sheikh Amri Abedi kwenda Moshi, wakati wakitembea huko ghafla Sheikh Kaluta Amri Abedi akawa haonekani tena, na mara likatanda giza kubwa mno. Maana ya kwanza ya njozi hiyo imetimia. Ni kweli zilipotangazwa habari za kifo cha Sheikh Kaluta Amri Abedi Sheikh Inayatullah Ahmad alikuwa Moshi katika shughuli za Mahubiri. Mara baada ya kupata habari alirudi haraka Dar es salaam na yeye ndiye aliyeongoza sala ya jeneza katika makaburi ya Jumuiyya ya Ahmadiyya yaliyoko Wailes Temeke.

Na dokezo la pili la kifo chake ni kwamba alipokuwa mgonjwa huko Ujerumani, aliona katika njozi aliona yupo peponi akiwa na njiwa wakizungumza Kiarabu.

Sheikh Kaluta Amri Abedi akumbukwa

Na Ayoub Mtekateka
Dar es Salaam

Sheikh Kaluta Amri Abedi ni Shujaa aliyesahaulika. Ukweli wa jambo hili ulidhihirika ndani ya ukumbi wa Karimjee, jijini Dar Es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu cha *Historia ya maisha ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi* kilichoandikwa na rafiki yake kipenzi katika fani ya utunzi wa mashairi, Mathias Eugene Mnyampala ambaye kwa sasa naye ni marehemu.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa serikali, viongozi wa dini, wasomi na wadau mbalimbali waliofika kushuhudia tukio hilo la kihistoria ambalo ndani yake ilikuwa ishara tukufu ya ukweli wa maneno ya Mwenyezi Mungu niliyoyanukuu hapo awali.

Uzinduzi wa kitabu hicho ulipata baraka za maombi ya kimya kimya yaliyoongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu wa jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Choudhry ambaye pia alipata fursa ya kutoa na kuelezea kwa ufupi falsafa ya maombi ya kimya kimya kwamba hiyo ilikuwa ni desturi ya Mtume Muhammad S.A.W na pia namna hiyo ya maombi hutoa fursa kwa watu kuomba jambo sawa na mtazamo wao juu ya tukio husika.

Katika tukio hilo lililoandaliwa kwa ushirikiano wa familia ya Sheikh Amri Kaluta na ile ya Mathias Mnyampala na wadau wengine, watu mbalimbali walipata fursa ya kuelezea kwa ufupi historia za namna marehemu hao walivyojitahidi katika kusaidia harakati za uhuru wa Tanganyika pamoja na juhudi zao za kukiendeleza na kukikuza Kiswahili kupitia mashairi na maandiko mbambali waliyoyaacha kama kumbukumbu na hazina isiyokwisha ya mashujaa hao kwa kizazi cha sasa na baadaye cha Watanzania.

Profesa Mulokozi wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, aliwasilisha mada aliyoiandika katika sura ya 'kijitabu' kidogo yenye kichwa cha habari: '*KALUTA AMRI ABEID, SHUJAA ALIYESAHAULIKA*', alimuelezea Sheikh Amri Kaluta kama ni mtu aliyekuwa mstari wa mbele katika kutetea kulinda na kuheshimu haki na maslahi ya wanyonge na wala hakuwa mbaguzi, bali alikuwa ni rafiki wa wote.Kwa upande wa kiimani, Profesa Mulokozi anamueleza Sheikh Amrin Kaluta ifuatavyo: "Kwa upande wa dini, Amri Abeid alikuwa ni mmoja wa waanzilishi na waenezaji wa imani ya Ahmadiyya katika Afrika Mashariki. ……Wale wanaomfahamu Kaluta Amri



Ayoub Mtekateka

Abeid, wanasema alikuwa ni Mcha Mungu sana, alijitahidi kuishi maisha ya unyoofu kama inavyoelekeza imani yake"

Uzinduzi wa kitabu hicho kilichoandikwa na marehemu Mathias Mnyampala kutimiza ahadi waliyowekeana marafiki hao wakati wa uhai wao. Inasemekana kuwa marafiki hao walikubaliana kuwa yeyote kati yao akitangulia kufikwa na umauti basi yule atakayebakia aandike kitabu cha historia ya maisha ya mwenziwe. Ndivyo alivyofanya Mnyampala katika kumuenzi rafikiye, Sheikh Kaluta. Kitabu hicho ni alama ya mapenzi ya dhati na urafiki wa kweli uliokuwepo baina ya nguli hao waliobobea katika fani ya utunzi na uandishi wa mashairi.

Mgeni rasmi katika tukio hilo alikuwa ni ndugu Kingunge Ngombale Mwiru ambaye katika hotuba yake alielezea namna ambavyo kuna umuhimu wa watu hao kuenziwa kwa kazi kubwa waliyaifanya ya kukikuza na kukiendeleza Kiswahili ambayo kwa sasa tunajivunia kuwa ni lugha ya kimataifa . Aidha, ndugu Kingunge aliweka wazi msimamo wake kwa wadau wa lugha ya Kiswahili na kusema kuwa anaunga mkono hoja ya Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia vyuo vikuu. " Lakini, ni Kiswahili cha namna gani?" Alihoji ndugu Kingunge ambaye alihitimisha hotuba yake kwa kukata utepe uliofungwa juu ya fungu la vitabu kuashiria kuzindua rasmi kitabu hicho kilichokuwa kikisubiriwa kwa hamu na wadau mbalimbali waliokuwepo ukumbini hapo.

Wakati tukio hilo likiendelea, ukumbi pacha wa jengo hilo la Karimjee kulikuwa na mkutano wa TAMISEMI uliowakutanisha wakuu wa mikoa na wale wa wilaya ambao nao walipata fursa ya kutazama hafla hiyo wakati wakipata kifungua kinywa nje ya ukumbi huo kupitia 'flat screen' iliyofungwa nje ya ukumbi kwa ajili wageni waliokosa fursa ya kuingia ukumbini.

Kabla ya hafla hiyo kufungwa rasmi, Sheikh Bakri Kaluta, ambaye ni mtoto wa marehemu Sheikh Amri alitoa salamu za shukrani kwa wageni waalikwa na kuelezea tukio la kushangaza la baba yake lilitokea mwaka 1953 wakati Sheikh Amri akisomea ubashiri nchini Pakistani ambapo siku moja aliwauliza wanafunzi wenzake "Itakuwaje mtakaposikia Amri Abeid amekuwa Meya wa jiji la Dar Es Salaam?". Wenzake hawakuitilia maanani habari hiyo kwani haikuwa na maana yeyote kwao. Lakini Sheikh Amri hakusema hivyo kwa matamanio yake bali ilikuwa ni njozi maalum aliyoiota ikimtaarifu juu ya nyadhifa atakakazoshika baadaye. Ndivyo ilivyokuwa, kwani baadaye alichaguliwa kuwa Meya wa kwanza Muafrika wa jiji la Dar es Salaam, miaka michache iliyofuata alichaguliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Waziri wa Sheria na baadae akawa Waziri wa Utamaduni wakati huo huo akiitumikia vyema Jumuiya.

Baada ya maelezo hayo ya kusisimua ya Shekh Bakri ambaye alitumia muda kwa iktisadi, mkuu wa kamati ya maandalizi ya hafla hiyo, Brigedia mstaafu, Mzee Adam Mbita alitoa shukrani kwa waalikwa na kisha kufunga rasmi kikao hicho kilichtumia saa tatu takribani

Ujumbe wa amani kwa Tanzania

Kutoka uk. 12

kuwa ni zenye kipato kikubwa ajabu. Mwandishi fulani wa kimarekani ameandika hivi:

"Kuna idadi kubwa ya watu hapa Marekani wanaotazama sinema kila siku. Kuna mamilioni ya mabinti wafanyao kazi na wanafunzi wanaotazama sinema usiku na mchana. Kwa hakika kuna mamilioni ya watoto na vijana ambao hawajui chochote cha mapenzi, kazi, shughuli za nyumbani, biashara, siasa, ulimwengu au chochote kingine isipokuwa kile wanachoelezwa na sinema hizo.

Kila aina ya dhambi iliyowahi kufanywa na watu wa nabii yeyote aliyepita, inafanywa na kuonyeshwa na sinema hizo, na kusambazwa na kufundishwa duniani kote, kwa mkupuo, kwa njia ya mitandao.

Kiasi kikubwa mno cha fedha kinatumika katika kutimiza ibada za miungu hiyo ya starehe na anasa kwa watu kuzamia ndani ya ulevi, kamari na uasherati, na matokeo yake nyumba nyingi zinabaki zikifilisika, watu wakizama ndani ya madeni, wengi wakibaki wanatota magerezani, wengine wakichukua njia ya mkato ya kujiua, kuyakwepa mateso yasiyovumilika yaliyosababishwa na miungu hiyo ya starehe na anasa. Kwa nini watu wanaendelea kujididimiza ndani ya gharama zote hizi zenye madhara makubwa ya ajabu? Sababu ni kwamba hamu ya starehe hizi huwa haipungui bali huongezeka, mungu bandia wa starehe ni lazima apate hisa yake.

Kama ilivyotokea katika zama za himaya ya Kirumi, ya Pompei, ya Sodom na Gomorrah, ndivyo hivyo inavyotokea leo katika zama zetu hizi. Matendo ya kishetani yaliyowaangamiza wanaume kwa wanawake katika siku za kale, yaliyoteketeza miji na mataifa, yanatendwa bila kificho, kwa mapana na marefu, duniani kote, na kuhamasishwa na hata kushinikizwa na baadhi ya mataifa yenye nguvu duniani kwa vitisho vya kukatiwa misaada.

Ufisadi umekuwa ni ugonjwa ulioenea duniani kote, saratani inayokuwa ndani ya majumba ya kizazi hiki cha mwisho, ikiwaangamiza, ikiwalemaza, ikiwaharibu na kuwavunjia kabisa mipango na matumaini yao. Uovu huu umeenea kiasi hiki kwamba haitakuwa imekosewa kama ikisemwa kuwa, huo ni mpango makhsus wa Ibilis, wa kuiangamiza dunia nzima na kuutokomeza kabisa ustaarabu wetu. Dunia inachupa, bila hiari, kwenye bahari iliyochafuka ya shida na simanzi, ikipigwa na mawimbi makubwa ya tamaa, wakati mawimbi yaendayo kasi ya hofu na ukataji tamaa, yakiivurumisha kuelekea kwenye miamba ya hatari iliyomo ndani ya giza la bahari yenye tufani.

Ingawa Dunia ina kila aina ya uvumbuzi wa sayansi na teknolojia, kila aina ya starehe ya kisasa, kila njia ya kupatia ladha ya kidunia, hakuna yoyote kati ya hizo inayoipunguzia hatari zinazoinyemelea. Watu wenye nguvu wanakwea na kuukamata usukani wa merikebu ya dunia bila ya mafanikio yoyote. Haiwatii tena, meli iko nje ya udhibiti ikitaraji huruma ya upepo na mawimbi yanayoipeleka kwenye maangamio. Mwanadamu hajawahi hapo kabla kuwa katika hali ya kutisha na kukatisha tamaa namna hii. Wanadamu duniani kote wanapiga mayowe ya kupatiwa safina mbadala ya kuwaokoa na tufani hilo. Je, Mungu Mwenye huruma Atawaacha viumbe wake wote wazame ndani ya bahari hiyo ya kutisha?

Hapana! Mungu ni Mwingi wa Huruma na Rehema. Alishatengeneza mazingira kwa wenye kutaka kusalimika. Alishamtuma Nuhu wa zama hizi aliyetengeneza safina ya kuwaokoa wanadamu kutoka kwenye dhoruba hii yenye kutisha mno. Amewatangazia wanadamu duniani kote kwa kuwaambia:

"Mafuriko ya ghadhabu za Mwenyezi Mungu yamefikia kileleni. Wale tu watakaokimbilia ndani ya safina ya Nuhu ndio watakaosalimika. Nitafuteni kwa ukweli na uaminifu wa moyo. Heri imo humu tu. Wanyama wakali wametapakaa kila mahali na ni kwangu tu unakopatikana mnara wa makimbilio wenye salama."

Huyu si mwingine ila ni Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., aliyeitangazia dunia kuwa yeye ndiye yule Masihi na Mahdi na Mujaddid wa karne ya kumi na nne aliyekuwa akisubiriwa sana kudhihiri na kuurekebisha ulimwengu. Ndani ya ukurasa wa 168 wa kitabu chake kiitwacho Kitaabul Bariyya ameandika kwamba:

"Ulipofika mwisho wa karne ya kumi na tatu, na karne ya kumi na nne ilipokaribia kuanza, basi Mwenyezi Mungu Akanipa habari, kwa njia ya Ilhaam (Wahyi), kwamba: wewe ndiye Mujaddid wa karne hii."

Na ndani ya kitabu chake kingine kiitwacho Izaalae awhaam uk. 632, kuna wahyi alioupata toka kwa Mwenyezi Mungu uliosema: yaani tumekufanya wewe kuwa Masihi mwana wa Mariamu.

Akijieleza zaidi Hadhrat Ahmad a.s. anasema ndani ya kitabu chake cha Arbain sehemu ya kwanza uk. 3 kwamba:

"Nimefahamishwa kwa Wahyi mtakatifu na uliotakaswa wa Mwenyezi Mungu kwamba mimi nimetoka Kwake nikiwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi wa ahadi, nami nikiwa ni mwamuzi wa hitilafu za nje na ndani. Hili jina langu lililowekwa kuwa Masihi na Mahdi, ni Mtume s.a.w. aliyenipa majina hayo, na halafu, Mwenyezi Mungu, kwa maneno Yake ya moja kwa moja, Amenipa jina hili hili na halafu hali ya sasa ya zama hizi imetaka pia jina langu liwe hili hili."

Hadhrat Ahmad a.s. alidhihiri katika mji mdogo wa Qadian huko India na kutimiza bishara za manabii kadhaa waliopita waliobashiri kuwa Nabii wa zama za mwisho atadhihiri katika sehemu hiyo ya Mashariki ya dunia.

Siku moja Mtume s.a.w. alisema kwamba Imam Mahdi atatokea katika eneo liitwalo Kaadiah (Qadian). Hii Hadithi yapatikana ndani ya kitabu kilichoandikwa mnamo mwaka wa 840 Hijriyya, yaani zaidi ya karne tatu kabla ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, kiitwacho Jawaahirul Asraar cha Hadhrat Sheikh Ali Hamza bin Ali Malik Twausii isemayo;

Mahdi atatokea katika eneo litakaloitwa Kaadiah na Mwenyezi Mungu Atamsadikisha. Atawakusanya masahaba zake wa nchi za mbali katika idadi ya watu wa Badri, watu mia tatu kumi na tatu.

Ndani ya kitabu kitakatifu cha dini ya Kihindu kuna bishara isemayo:

"Kuna mtakatifu fulani atadhihiri na kuonyesha ushujaa wake katika sehemu iitwayo Qadun." ambayo kwa hakika ndio Qadian. (Athar ved, kand ya 20, saukat ya 97, mantar ya 3).

Halikadhalika ndani ya kitabu cha Masingasinga cha Janam Saaki bhai bhala waali waddii saaki uk. 251 kuna riwaya isemayo kwamba Bwana Mardane alimuuliza hivi Guru Nanak:

"Guru sahib! Je kutakuwepo na Guru mwingine atakayekuwa mtakatifu zaidi kuliko Kabir Bhagat? Kama atakuwepo ni wapi na lini?" Hapo Guru Nanak akasema: "Guru ajaye atakuja miaka 100 baada yetu, atakuwa ni mmiliki wa ardhi na atatokea katika maeneo ya Batala." Qadian imo ndani ya eneo miliki la Batala.

Yesu pia alisema kuwa atatokea Mashariki kama alivyosema: "Kwa maana, kama vile umeme utokavyo Mashariki na kuonekana hata Magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adam." Yesu aliitoa bishara hii wakati akiwa Jerusalem. Na Qadian, mji aliozaliwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., uko upande wa mashariki wa Jerusalem.

Hata Mtume Muhammad s.a.w. alisema kuwa Masihi Isa bin Mariam ataibukia kwenye mnara mweupe uliopo Mashariki ya Damascus. [Ibni Maajah]. Ukiitazama ramani utaiona Qadian ikiwa upande wa Mashariki kabisa wa Damascus.

Imam Bukhari ameandika ndani ya kitabu chake cha Historia kwamba Hadhrat Anas bin Malik r.a. alisimulia kwamba siku moja Mtume s.a.w. alisema kwamba "kutakuwepo na kundi litakalopigana vita ya Jihadi huko India, nalo litakuwa pamoja na Imam Mahdi ambaye jina lake litakuwa ni Ahmad."

Halafu ndani ya kitabu cha Bihaarul Anwaar jal. 13 na Abuu Daud jalada la 2 bab khurujul Mahdi, na hata ndani ya Ibnu Maajah, Mtume s.a.w. amenukuliwa akisema kuwa: "Watu watatokea Mashariki watakaotoa taarifa kuhusiana na Mahdi ambaye ndiye atakayekuwa kiongozi wao." Yaani watamuunga mkono na kumsaidia.

Bishara hizi za manabii mbali mbali waliopita katika zama na maeneo tofauti, ziliandaliwa kuja kuwaongoza watu wa dini tofauti, wa zama zetu hizi, kumtambua mwokozi wetu wa kuja kutuingiza katika amani na upendo. Mwenyezi Mungu Alimfunulia Mwokozi huyo, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., habari nyingi za mambo yatakayotokea baadae, yakiwemo ya majanga yatakayoisibu dunia yetu ya leo.

Katika wakati wake hakukuwa na nchi yoyote ya Mashariki iliyoweza kukabiliana na nchi zenye nguvu za Magharibi. Lakini mnamo mwaka 1904, alifunuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa nchi fulani za Mashariki zitaibuka na kuwa nchi zenye nguvu na kuweza kukabiliana na nchi zenye nguvu za Magharibi. Haukupita muda mrefu baada ya kutolewa bishara hii, nchi ya Mashariki ya Japan ikaishinda Urusi katika vita na kuwa miongoni mwa nchi zenye nguvu duniani.

Japan nayo ikashindwa katika vita kuu ya pili ya dunia na China ikaibuka kuwa miongoni mwa nchi za Mashariki yenye nguvu duniani. Kuibuka kuwa mataifa yenye nguvu kwa mataifa haya mawili ya kimashariki, kukabadili mwelekeo wa historia na athari zake zimeendelea kuenea duniani kote, na leo hii China na Japan ni nchi tajiri sana na zenye nguvu kubwa duniani.

Mnamo mwaka 1905, Hadhrat Ahmad a.s. alipata ufunuo mwingine uliofahamisha kuwa Kaisari wa Urusi pamoja na familia yake na serikali yake yote itakumbwa na msiba na madhila makubwa sana na kuangamizwa kabisa. Ni ajabu kwamba ndani ya miezi michache tu kikaundwa chama cha siasa huko Urusi kilichokuja kuuangamiza kabisa utawala wa mfalme Kaisari wa Urusi miaka 12 au 13 baadae. Chama cha kikomunisti kikashika hatamu na kumng'oa Mfalme wa Urusi na hatimaye kumuua baada ya kumdhalilisha mno pamwe na familia yake.

Ilibashiriwa na mitume waliopita kuwa katika siku zetu hizi za mwisho wa dunia, wakati wa kudhihiri Imam Mahdi a.s., dunia itagawanyika katika makundi mawili yenye kuhasimiana. Yatakuwa ni mataifa yenye nguvu sana kiasi ya kwamba hakuna Taifa lolote litakaloweza kupambana nayo. Hatimae, mataifa hayo ya Magharibi na Mashariki, yatapigana vita na kuangamia.

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Imam Mahdi, Mirza Ghulam Ahmad a.s., alifahamishwa na Mwenyezi Mungu na kuutangazia ulimwengu kuwa vitatokea vita vikuu vitano vya dunia. Kuhusiana na vita kuu ya kwanza ya dunia alitangaza kwamba itakuwa ni vita itakayotokea kwa ghafla mno kiasi ya kuishangaza dunia. Alibashiri kuwa watakaokutwa na vita hiyo wakiwa safarini watapata shida mno, mito itageuka myekundu kwa damu, vijana wataonekana kama wazee kutokana na shida na misukosuko ya vita hiyo, milima italipuka, watu watawehuka kutokana na hofu ya vita, na huo utakuwa ndio wakati wa kuangamia kwa Kaisari wa Urusi, mbegu za ukomunisti zitapandwa wakati huo, manowari za kivita zitawekwa katika hali ya tahadhari, vita kubwa ya baharini itapiganwa, falme zitapinduliwa na miji itageuka kuwa makaburi. Vita hii ikaja tokea miaka sita baada ya Hadhrat Ahmad a.s. kufariki, kwani alimwomba dua Mwenyezi Mungu kuwa Amfishe kabla ya kutokea kwa vita hiyo. Hayo yote yaliyotabiriwa naye yakatokea vivyo hivyo.

Pia alitabiri janga lingine kwa sura ya vita kuu ya pili ya dunia itakayokuwa ni kubwa na yenye maafa zaidi kuliko ile ya kwanza. Vita itakayoibadili ramani ya dunia na kubadili mwelekeo wa watu. Ukomyunisti ulitabiriwa kupata nguvu wakati huo na kuwa taifa lenye kuogopeka, mataifa mengi yatakuwa chini ya himaya yake.

Na ndivyo ilivyotokea, kwani baada ya vita kuu ya pili ya dunia, nchi nyingi za Ulaya ya Mashariki zikawa za Kijamaa na kufuatiwa na watu milioni mia saba wa China na nchi nyingi za Ulimwengu wa tatu zikiwemo za Afrika, Asia na za Amerika ya Kusini. Hapo Dunia ikagawanyika katika kambi mbili zenye uadui na silaha za kutisha.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Kujiuzulu kwa Papa Benedict xvi

Kutoka uk. 12

aliyemchagua, angalau tungepata imani kidogo ila tutajiuliza swali alifanya kosa gani hadi Mungu ampe amri hiyo? Lakini hilo halisemwi yanasemwa yasiyoingia akilini. Hapa kuna jambo kubwa tunafichwa ili historia ipotee na ndiyo maana tunalazimika kutumia akili zetu ili historia isiwekwe pabaya.

Kanisa katoliki ni taasisi kubwa hapa duniani yenye mtandao mpana sana na ushawishi mkubwa na wa hali ya juu wa kisiasa. Na ndiyo maana Kiongozi wa kanisa hilo anaishi Vatican nchini Italia, mji ambao una hadhi sawa na nchi na kupata uwakilishi wa kibalozi kote duniani. Kwa upande wa kidini Papa anawawakilishi katika kila nchi wanaoitwa Makadinali na maaskofu na vyeo vingine kadhaa vya chini.

Kwa miaka mingi sana toka kuanzishwa kwake, Kanisa Katoliki limegubikwa na mlolongo wa kashfa, hasa ukizingatia kuwa baadhi ya kashfa zinasababishwa na mfumo mzima wa uendeshaji wa kanisa, sera, mitazamo, itikadi, imani na siasa za kanisa hilo zimepeleka madhara kwa watu wengi duniani, hivyo kuwa Papa kunataka moyo wa chuma.

Ukweli ni kwamba Kanisa Katoliki kwa miaka mingi iliyopita lilihusika katika baadhi ya nchi kupanga, kuratibu na kuweka viongozi wa nchi mbalimbali ambao walifanya dhuluma kubwa kwa watu wengi na kugharimu uhai wa wanadamu wengi wasio na hatia. Kuteka nchi na kuwalazimisha watu wafuate imani za Kanisa hilo ilikuwa ni mipango ya muda mrefu ya Kanisa hilo. Wapo viongozi walioongoza ubakaji na kunajisi watoto wadogo kwa sababu ya itikadi za maisha ya kitawa ya Kanisa hilo ambayo inakataza kabisa kuoa. Sote tunakumbuka kuwa Papa John Paul II aliwahi kuomba radhi kwa niaba ya Kanisa Katoliki kwa makosa mbalimbali ikiwemo la Kunajisi watoto wadogo kulikofanywa na watawa wa kanisa hilo miaka ya nyuma.

Papa Benedict XVI toka aingie madarakani, amekumbana na aina mpya ya kashfa za Kanisa Katoliki ambazo yeye mwanzoni aliziita kuwa ni changamoto, kama za ushoga, usagaji na ndoa za jinsia moja. Kanisa Katoliki na tuhuma za uhusiano wake na mtandao wa Freemasons, maaskofu kudai haki ya kuoa na mengine mengi. Changamoto hizi zimegeuka kuwa matatizo makubwa kwake na kuona ni bora ajiuzulu ili Kanisa Katoliki lisisambaratike mikononi mwake. Imeelezwa kuwa katika mambo yaliyomsukuma kujiuzulu ni jinsi kasi ya ushoga inavyoshamiri ndani ya kanisa hilo na usaliti unaozidi wa baadhi ya Maaskofu kufunga ndoa nje ya nidhamu ya Kanisa hilo. Mara kadhaa amewahi kunukuliwa akisema anaumizwa na ajenda hiyo mbaya inavyoshamiri Kanisani, na hivyo kuonyesha kuwa hana jipya la kufanya, amekata tamaa na hatimaye kuamua kujiuzulu. Kama sababu za kujiuzulu kwake zitabaki kuwa siri kubwa ya Kanisa ipo siku itawekwa hadharani kama wanavyoweka makosa ya nyuma yaliyofanywa na Kanisa hilo.



Picha ya Papa Benedict xvi kama ilivyowasilishwa na baadhi ya magazeti hapa nchini ikijaribu kuonyesha uhusiano wake na masuala kadhaa ya kisiasa na kiimani duniani

Mahubiri yapambamoto chuo kikuu cha Morogoro

Kutoka uk. 12

kutualika tena siku nyingine. Maandalizi ya mtihani wa kumaliza muhula yaliwafanya wakose muda wa kutualika tena hadi wanakwenda likizo.

Mwezi Machi chuo kilipofunguliwa Mwenyekiti bwana Adam alinieleza kuwa wanatuhitaji tena. Alinidokeza kuwa baadhi ya wanafunzi wanaomba nisiende na Sheikh wakidai ni maji marefu na si saizi yao. Nilimfahamisha kuwa nitakwenda nae na kumwambia kuwa wanaotoa hoja hizo ni wapenda ubishi na si watafuta elimu.

Nilienda na Sheikh kwa mara nyingine katika hostel za cheers na kufanya mazungumzo na wanafunzi hao. Baadhi ya wanafunzi waligoma kutokea kutokana na ujio wa Sheikh lakini mazungumzo yaliendelea kama kawaida. Siku hiyo hali ilikuwa tofauti kwani ulizuka mjadala mzito kutoka katika sura 61:7 na kuchukua muda mrefu hadi mwisho wa mazungumzo. Kutokana na Mtume aliyetajwa katika aya hiyo wao walidai ni Muhammmad na si mwingine. Sheikh alipangua hoja yao kwa kumalizia aya ya nane ya sura hiyo inayosema kuwa sifa ya nabii huyo ataitwa ndani ya uislamu, sifa ambayo Mtume Muhammad (s.w.a) hana. Kujitoa katika kigingi hicho walihoji je, baada ya Issa alikuja Ahmad au Muhammad?

Sheikh aliwapa mfano katika sura 46:31 kutengua hoja yao, ndipo baadhi yao wakataka kuvunja mazungumzo lakini wenzao waliwapuuza na kuwazuia hali iliyofanya mazugumzo yaendelee. Muda wa magharibi ulipokaribia mwenyekiti alisitisha kikao huku wengi ao wakiwa bado wana shauku ya kuuliza maswali. Kuna baadhi ya watu walijaribu kuzuia mazungumzo hayo wakidai mwenye hosteli hajaruhusu. Kwa hamasa ya kutafuta elimu wanafunzi walihoji, mbona mabishano ya soka huwa hayazuiliwi sembuse mazungumzo ambayo jina la Mwenyezi Mungu na Mtume wake linatajwa.

Kiu ya kujua zaidi juu ya Ahmadiyya ilizidi kushika kasi miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro. Hoja juu ya utume kuendelea na kifo cha Nabii Issa (as) zilipata mashiko makubwa miongoni mwao. Hali hiyo iliwapelekea kila wanaponiona kunihoji juu ya masuala mbalimbali ya dini katika msimamo wa kiahmadiyya. Nililazimika kutumia muda mwingi nikiwa chuoni kuhubiri. Hali hiyo ilipelekea nipewe majina mbalimbali na wanafunzi wenzangu chuoni kama vile; Ahmadi Mirza, Qadiani, Ahmadiyya n.k. Wapo waliyokuwa wakinidhihaki ya kwamba nalipwa fedha na wahindi kwa kufanya kazi hiyo. Wengine wakahukumu dini ya Kiislamu makao yake makuu hayawezi kuwa Uingereza,ilimradi tu walikosa hoja za msingi.

Majadiliano ya juu ya hoja mbali mbali za kiahmadiyya yakachukua sura mpya katika kijiwe cha siasa kilichopo karibu na geti kuu la Chuo hiki ambacho ni pekee cha Waislamu hapa nchini kilichosheheni wasomi kutoka maeneo mbalimbali duniani. Kijiwe hicho ambacho inaaminika kuhudhuria hapo ni zaidi ya shahada, kina kusanya wanafunzi wengi wanaosifika katika kutafakari mambo kwa kina. Hivi karibuni kimebatizwa jina na kuitwa kijiwe cha wanaharakati. Mtu yeyote chuoni hapo anayejitambulisha kuwa mwanaharakati na si mwanachama wa kijiwe hicho watu humuona kama kioja.

Majadiliano marefu baina yao yaliwafanya wapate hamu ya kutembelewa na Sheikh wa kiahmadiyya ili awatoe uvulivuli na ukakasi juu ya masuala waliyokuwa wana shaka nayo. Tarehe 10/04/2013 mnamo majira ya saa kumi na nusu ujumbe wa Ahmadiyya ukiongozwa na Sheikh Bakri uliwasili katika kijiwe cha wanaharakati hatua chache kutoka geti kuu la chuo.

Baada ya salamu na utambulisho, mazungumzo yalianza rasmi chini ya Mwenyekiti Halfani Mshana mwanafunzi wa mwaka wa pili katika shahada ya kwanza ya sanaa na ualimu. Alhaji Sheikh Bakri Kaluta alipewa nafasi kueleza kwa ufupi juu ya Ahmadiyya. Baada ya maelezo mafupi ya Sheikh wanafunzi walipata fursa ya kuuliza maswali na Sheikh aliwajibu kwa ustadi mkubwa kwa kuzingatia kiwango cha elimu yao. Alitoa ushahidi wa hoja na dalili kutoka katika Qur'ani Tukufu na hadithi za Mtume Muhammad (saw). Maswali mengi yalizama katika yakini ya Seydna Ahmad (a.s) yaani kuendelea kwa utume na kifo cha Nabii Issa (a.s).

Saa kumi na mbili na nusu jioni Mwenyekiti aliahirisha kikao akiwaomba wanafunzi wenzake wakajipange kwa kutafuta ushahidi wa kutosha juu ya hoja wanazozipinga. Wote walikubaliana na rai ya Mwenyekiti wakaahidi watakapokuwa tayari watatualika tena. Alhaji Sheikh Bakri Kaluta aliwasihi kuacha ushabiki na jazba katika kusoma masuala ya dini na badala yake kutafakari ukweli kwa hoja na dalili. Pia Sheikh aliwaalika ofisini kwake wakati wowote watakapopata wasaaa wa kufanya hvyo.

Pamoja na Alhaji Shekh Bakri ujumbe wa Ahmadiyya ulikuwa na watu watano.Wengine ni bwana Nasiri Mnungu, Hamisi Madua, Hamidu Salehe, Maliki Ramadhani na Lutufu Mbanga ambaye ndiye mwandishi wa habari hizi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie ujumbe wa Masihi ufike ndani kabisa ya chuo utakase nyoyo zao na kuzaa matunda yaliyo mema. Amin.

TANGAZO KUTOKA KITENGO CHA UTAFITI WA VITABU RABWAH PAKISTAN

Kitengo cha Utafiti wa vitabu kilichopo Rabwah Pakistan kinapenda kuwatangazia wanajumuiya wote kwamba kitengo hicho kimepewa jukumu la kuandaa orodha kuu "Master Catalogue" ya vitabu vyote vya Jumuiya na vile vilivyoandikwa na Wanajumuiya.

Hivyo Mwanajumuiya yeyote aliyewahi kuandika au kuchapisha kitachu cha aina yoyote kwa jina lake kuanzia mwaka 1889, anaombwa apeleke taarifa hizo kwenye kitengo hicho ili kitabu chake kiweze kuingizwa kwenye orodha hiyo kuu.

Taarifa zinazotakiwa kutumwa ni:

Jina la kitabu, Mwandishi/Mfasiri, Toleo, mahala kilipochapishwa, tarehe ya uchapishaji, Mchapishaji, idadi ya kurasa, ISBN, Lugha na Maudhui.

Aidha mwanajumuiya yeyote aliye na kitabu chochote cha Jumuiya cha zamani naye anaombwa awasiliane na kitengo hicho.

Tafadhali wasiliana nao kwa:

Incharge Research cell, P. O. Box #14 Chenab Nagar (Rabwah), Pakistan
Ph. office. 0092476214953,
Res: 0476214313
Fax: 0092476211943
Email: research.cell@saapk.org

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jumaduth Thani 1434 AH | Aprili 2013 | Shahadat 1392 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

IImesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Kila mmoja wenu ni mchungaji na kila mmoja wenu ataulizwa kuhusu raia wake. Amiri ni mchungaji. Na mtu ni mchungaji wa watu wa nyumbani mwake. Na mwanake ni mchungaji wa nyumba ya mumewe na watoto wake. Basi kila mmoja ni mchungaji na kila mmoja ataulizwa kuhusu raia wake. (*Bukhari*)

Ujumbe wa amani kwa Tanzania

Hotuba iliyotolewa na Sheikh Bakri Kaluta katika mkutano wa amani - Morogoro 2013

Mungu ni Upendo, Mungu ni Amani, Upendo hauwezi kuzaa chuki, na Amani haiwezi kuelekeza kwenye vita. Ndio sababu kauli mbiu ya Jumuiya yetu imedumu kuwa Upendo kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Leo dunia inapigwa na bumbuazi kwamba ni nini kimeikumba jamii yetu kiasi ya kwamba upendo na amani vinatoweka kwa kasi miongoni mwetu na hatimae kuibuka chuki inayoelekeza kwenye vita. Ni nini kimesababisha hali hii. Majibu tofauti yanatolewa na jamii mbali mbali, kila mmoja katika anga zake. Hebu tuizamie kwa kina hali hii tujaribu kuibuka na sababu zenye thamani zitakazoweza kuinusuru jamii yetu ya Tanzania, Afrika na dunia nzima.



Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood (wa pili kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na wabashiri wa Mkoa wa Morogoro wakati wa Mkutano wa amani uliofanyika tarehe 7/4/2013. Wa mwanzo kushoto ni Sheikh Bakri Kaluta - mwandishi wa makala hii.

Hakuna shaka kwamba mwanadamu ameshindwa kuidhibiti tamaa ya kuziabudu kazi alizozitengeneza kwa mikono yake mwenyewe, na amempuuza Mungu Yule ambaye msukumo wa mafanikio yote huchimbukia Kwake. Chini ya shinikizo la kuyahangaikia maisha ya kisasa yanayoboreshwa na kurembeshwa kiajabu kutokana na elimu ya Syansi na Teknolojia, wazo la Mwenyezi Mungu limetoweka kabisa ndani ya akili za watu wengi sana, ni sawa tu na kusema kuwa wazo la Mwenyezi Mungu halipo kabisa ndani ya akili zao.

Mungu bandia wa dhahabu amepata wafuasi wake walio waaminifu kabisa, Tamaa imedumu kupata wafuasi wengi wa kumuabudu kwenye hekalu lake. Takriban dunia nzima imeinama kwa heshima na taadhima mbele ya mungu bandia wa ulafi, umero na uchoyo.

Kamari, kama vile alivyo mungu Mammon, mungu bandia wa ulafi, umero na uchoyo, ni mungu wa majonzi na simanzi. Imeziangamiza nyumba zisizo na idadi. Kila siku kamari inatoa matumaini ya uongo ya kuneemeka kiulaini ndani ya mioyo isiyo na idadi, na hatimaye kuwatumbukiza, bila huruma, ndani ya mashimo marefu ya majonzi. Inadhoofisha nguvu kazi, inaiharibu juhudi ya kweli, inazalisha hali ya kutotosheka, ya kukata tamaa na ya kuvunja moyo. Hizi ni hali zenye kuufukuza upendo na kuikaribisha chuki isiyovumilia hata kidogo manukato ya amani, bali ni yenye kuvutiwa mno na harufu itishayo ya damu.

Mungu mwingine wa bandia anayeabudiwa siku hizi ni mungu wa starehe na anasa anayesababisha shughuli za mambo haya ya starehe na anasa

Endelea uk. 10

Mahubiri yapambamoto chuo kikuu cha Waislamu Morogoro

Na Lutufu A. Mbanga - Morogoro

Mjadala wa kihistoria ilibidi ufanyike mwaka jana mwanzoni katika Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro baina ya Sheikh ambaye ni mwanafunzi wa chuo hicho dhidi ya Waahmadiyya. Kutokana na sababu mbalimbali mjadala huo ulishindikana kufanyika. Moja ya sababu kubwa ikiwa kutoonekana kwa Sheikh ambapo hata alipotafutwa kwenye simu yake hakupatikana.

Kushindikana kwa mjadala huo haukuwa mwisho wa harakati za mahubiri katika chuo hicho zilizokuwa chini ya Majlis Khudamul –Ahmadiyya Morogoro mjini. Kutokana na mazungumzo ya kidini kati ya mwandishi wa habari hizi na wanafunzi wenzake chuoni hapo, wanafunzi hao walishikwa na shauku kubwa ya kufahamu zaidi juu ya Ahmadiyya. Miongoni mwa hoja zilizoteka hadhira kubwa miongoni mwao ni juu ya utume kuendelea na kifo cha Nabii Issa (a.s).

Shauku ya wanafunzi hao ilienda sambamba na haja ya Alhaji Sheikh Bakri Kaluta ya kufikisha ujumbe wa Masihi



Mwalimu Lutufu Abdallah Mbanga, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro.

katika kila kona. Nilipofika Morogoro Oktoba 2011 kuanza masomo yangu chuoni hapo, Alhaji Sheikh Bakri alinitaka nijitahidi kadri ya uwezo wangu ujumbe wa Masihi ufike chuoni hapo. Aliniahidi wakati wowote atakapohitajika yupo tayari kufika ili kutimiza ile bishara aliyopewa Seydna Ahmad na Mwenyezi Mungu ya kwamba "Nitafikisha ujumbe wako katika kila pembe ya dunia".

Mnamo Januari mwishoni, majira ya saa kumi kasoro alasiri nilipokea simu kutoka kwa mwanafunzi Ramadhani Bhatia, anaeishi hosteli za cheers zilizo nje kidogo ya chuo. Alinieleza ya kwamba wananihitaji kwa ajili ya kupata ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali za kiahmadiyya. Nilifika msikitini kwa ajili ya sala ya alasiri na baada ya sala nilimueleza Sheikh juu ya haja ya wanafunzi hao na kumuomba tuongozane pamoja. Sheikh alithibitisha kauli yake kwa vitendo. Kwa bashasha na furaha iliyozidi kifani alifunga ofisi tukaaongozana hadi hostel za cheers.

Mazungumzo yaliyokuwa yakiongozwa na mwanafunzi mwenzao bwana Adam, yalikuwa mazuri na kuvuta hisia za pande zote mbili. Sheikh alipewa nafasi ya kueleza kwa muhtasari juu ya historia ya Ahmadiyya na shabaha ya kuanzishwa kwake. Baada ya maelezo ya Sheikh wanafunzi walianza kuuliza maswali, ambayo sheikh aliyajibu kwa hoja na dalili kutoka katika Qur'an Tukufu na hadith za Mtume Muhammad (s.a.w). Kama ilivyo kawaida maswali mengi yalijikita katika utume kuendelea na kifo cha Nabii Issa (a.s). Ilipofika majira ya saa kumi na mbili na nusu jioni mwenyekiti alisitisha mazungumzo hayo na kutuahidi watajipanga na

Endelea uk. 11

Kujiuzulu kwa Papa Benedict xvi na kashfa za Kanisa Katoliki

Pazi Mazongera, Dar es Salaam

Kanisa Katoliki limeingia katika historia mpya toka kuanzishwa kwake mamia ya miaka iliyopita. Wana historia wanatueleza kuwa aliwahi kujiuzulu Papa miaka 600 iliyopita bila ya kuweka wazi sababu za kufanya hivyo huko nyuma. Aidha wana historia hawa wanataka kurudia kosa la kutoweka bayana katika kumbukumbu za leo sababu za kujiuzulu kwa Papa Benedicto XVI kwa makusudi ili kizazi cha baadaye kisiwe na uhakika ya sababu hizo. Sababu ambayo haina mashiko ni afya na umri mkubwa alionao Papa ndizo zimemsukuma afikie maamuzi mazito kama hayo ya kujiuzulu. Lakini tumeona Papa wengi hata aliyemtangulia Papa John Paul II aliongoza kanisa katika hali ya uzee, ugonjwa na uzezeta wa hali ya juu na kupoteza kumbukumbu na alikufa akiwa Papa, kwani kuwa Papa ni zaidi ya heshima ya kawaida ambayo kanisa linampatia binadamu katika ulimwengu huu hata ikibidi kufa nao.

Kwa kuwa katika utaratibu wa kumchagua Papa umegubikwa na kile wanachokiita ucha Mungu wa hali ya juu, na wanasema ule uchaguzi ni wa Mungu mwenyewe hata kufika mahali kutueleza kuwa Papa ni mwakilishi wa Mungu hapa duniani. Kama kweli ni maradhi ndiyo yanayomfanya Papa kushindwa kuongoza kanisa vizuri, Je huyo Mungu aliyemchagua ameshindwa kumsaidia kumponya au angalau kumpa afya nzuri ili atimize japo miaka kumi ya kuongoza Kanisa lake hilo lenye Waumini wengi duniani? Ni Mungu gani huyo anayeweza kumuacha Kiongozi aliyemchagua mwenyewe afya yake izorote kwa muda mrefu, apoteze kumbukumbu na ashindwe hadi kuongoza misa, ashindwe kula chakula na kutotambua hatima ya Kanisa lake na anaowaongoza ilihali bado yu hai? Inawezekana jibu lake ni rahisi kwamba, kuwa Papa si kazi kubwa unakuwa mtu unaewakilisha kundi kubwa la watu na ni nembo tu ya kuwepo kwa watu hao duniani na mambo yote yanaweza kufanywa na wengine bila hata Papa kujua kama ilivyotokea kwa Papa John Paul II ambaye baadhi wetu tulimuona alivyokuwa.

Wana historia wasisahau kutueleza ya kwamba umri si kigezo cha kumchagua Papa, ndiyo maana Papa Benedict XVI alichaguliwa akiwa na miaka zaidi ya sabini. Je uchaguzi wa Mungu uligubikwa na kutotambua umri wa anaemchagua? Bila shaka uwezo wa Mungu huyo utakuwa na mashaka makubwa, ya kusahau hata umri wa kipenzi chake. Siku chache kabla ya uchaguzi Papa Benedict XVI aliwahi kusema angependa Papa wa kipindi hiki atoke Bara la Afrika au Asia! Hilo lilishindikana kwani Papa ametoka Amerika ya Kusini. Chaguo la Mungu limeshindwa hata kuwa na ushawishi kwa Mungu wake ili neno lake litimie!

Kwa upande mwingine nimekuwa nikipata tabu sana hasa kuona mtu aliyepewa dhamana kubwa na Mungu na akaamua kuacha dhamana hiyo kwa sababu ambazo bado hazina mashiko. Hivi kweli umeshika ahadi na Mungu ya kuongoza Kanisa lake na Wakristo wengi zaidi hapa duniani na unaweza kuacha kufanya kazi zake? Au tuambiwe kwamba Mungu amemuamuru Papa ajiuzulu kwani ni yeye ndiye

Endelea uk.11